# Jamii iliyounganishwa

## Kitini cha mafunzo kwa mtandao wa simu

Mwongozo wa kufundishia watu mafunzo
ya msingi kwa mitandao ya simu



Copyright © 2017 GSM Association

GSMA inawakilisha kile wakipendacho waendeshaji wa mtandao ulimwenguni, ikiwaunganisha zaidi ya waendeshaji 800 wenye zaidi ya makampuni 250 wenye mtandao mpana wa mfumo wa simu za mkononi, ikiwa pamoja na simu za mkinoni na watengezaji wa nyenzo nyingine, wasambazaji wa mahitaji na kampuni za intaneti, lakini pia mashirika mengine sambamba na sekta za viwanda. GSMA pia inaandaa makongamano makubwa ya viwanda ulimwenguni kama vile Mobile World Congress, Mobile World Congress Shanghai na Mobile 360 Series Conferences.

Kwa mawasiliano zaidi tembelea mtandao wa GSMA
www.gsma.com

Fuatilia GSMA kwenye Twitter: @GSMA

## GSMA Jamii Iliyounganishwa

GSMA jamii iliyounganishwa ni program ya GSMA ya kuunganisha watu. Inafanya kazi na mtandao wa simu ya mkononi, utumiaji, ujuzi wa kidigitali na maudhui halisi katika kufikia uwanda mpana wa intaneti ya simu.

Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea:
www.gsma.com/mobilefordevelopment/programmes/connected-society

Au wasiliana nasi kwenye: connectedsociety@gsma.com

# Yaliyomo


**Utangulizi** **4**
Utangulizi kwenye kitini hiki 4
Nini kimo ndani ya kitini hiki 6
Mtizamo wa maudhui ya mafunzo 8
Kitini hiki kinaweza kutumikaje? 9

**Mafunzo ya kipimo cha kifurushi** **10**
Jinsi ya kutumia mafunzo ya kipimo cha kifurushi 12
**Intaneti ya simu ya mkononi ni nini?** 14
**WhatsApp** 16
**YouTube** 18
**Google** 20
**Wikipedia** 22
**Facebook** 24
**Usalama** 26
**Gharama** 28

**Mafunzo ya kina** **30**
Jinsi ya kupanga mafunzo yako 32
Dondoo kwa wakufunzi 33
Jinsi ya kutumia mafunzo ya kina 34
Orodha ya vipengele vya mafunzo 35
Moduli 1: **Utangulizi** 36
Moduli 2: **WhatsApp** 46
Moduli 3: **YouTube** 58
Moduli 4: **Google** 70
Moduli 5: **Wikipedia** 84
Moduli 6: **Facebook** 94

**Rasilimali: Vipeperushi na machapisho** **104**

Nembo mbalimbali
Vyeti

# Utangulizi wa kitini

Simu za mkononi zina matumizi zaidi ya kupiga simu. Watu wengi ulimwenguni huzitumia kwa intaneti. Matumizi ya Intaneti yana faida kubwa kwa mtumiaji, hata hivyo yanahitaji ujuzi maalum na utaalam wa kutumia vyema simu za mkononi. Hii ni kumaanisha kwamba watu wanaokosa ujuzi na uelewa wa matumizi hayo hawataweza kutumia vilivyo huduma hiyo.

## Kitini hiki kina lengo gani?

Kijarida hiki ni kwa ajili ya mashirika ya mitandaoni, mashirika yasio ya kiserikali, mashirika ya kimaendeleo na serikali zinazohitaji kutoa mafunzo ya msingi juu ya elimu ya mtandao.

Nyenzo na vitendea kazi vinavyotolewa hapa vinawapa wakufunzi mwongozo wa kuonesha thamani na utendaji kazi wa mtandao. Matokeo yake, wanafunzi huelewa zaidi jinsi ya kutumia mtandao. Tunaamini kwamba hii itasaidia kuongeza ufahamu na kuboresha huduma ya matumizi ya mtandao itakayotolewa.

Mafunzo yanayotolewa kwenye kitini hiki, yanawalenga wale wenye ujuzi mdogo au wasio na ujuzi kabisa wa mtandao. Kinakusudia kufundisha wale wanaotaka kujifunza maana ya mtandao na jinsi ya kuwasiliana na vilevile jinsi ya kutafuta kwenye mtandao. Kitini hiki si mwafaka kwa watu wasio na uzoefu wa kutumia simu za mkononi, na hakina maelezo ya msingi kama vile jinsi ya kupiga simu au kutuma ujumbe. Kwa sababu hiyo kitini hiki hakina maelezo ya jinsi ya kupakua program au kufungua akaunti ya barua pepe, kwavile mlolongo wote huo ni usumbufu kwa wasiokuwa na ujuzi wa mambo ya mtandao. Na vilevile, haikukusudiwa kwa wale wenye uelewa wa mtandao.

Ingawaje kitini hiki kimelenga watu wa jimbo la Maharashtra, India, tuna uhakika kwamba kinaweza kutumika sehemu nyingine za nchi. Zaidi ya hayo, kinaweza kutumika kukidhi mahitaji ya watu wa nchi nyingine kwa kulingana na mwongozo wake.

# Utangulizi wa kitini

### ”Jinsi ya Kuongoza” ninini’?

“Jinsi ya kuongoza” lazima iendane na nyaraka hii, ili kumwezesha mkufunzi katika nchi yoyote ile aweze kuendeleza na kufikisha mafunzo maalum ya mtandao kwa walengwa wake.

Mwongozo unatoa mapendekezo jinsi ya kufundisha vipengele vyenye maana kwa walengwa maalum.

“Jinsi ya kuongoza”pia inajumuisha mifano kadhaa iwezayo kutumika kama nyongeza ya taarifa kutoka kwenye kitini hiki. Tunapenda kuwashawishi watumiaji wote wa kitini hiki kupitia na kutumia yaliyomo kwenye “Jinsi ya kuongoza” ili kukamilisha mafunzo yao vyema

“Jinsi ya kuongoza” pia inajumuisha mifano kadhaa iwezayo kutumika kama nyongeza ya taarifa kutoka kwenye kitini hiki. Tunapenda kuwashawishi watumiaji wote wa kitini hiki kupitia na kutumia yaliyomo kwenye “Jinsi ya kuongoza” ili kukamilisha mafunzo yao vyema.

# Nini kimo ndani ya kitini hiki?

Kitini hiki kinatoa utangulizi juu ya matumizi ya intaneti kwenye simu katika hatua ya awali kwa matumizi ya smartphone. Kinafanana na safari ambayo humpa mwanafunzi ujuzi wa awali juu ya mawasiliano, kwa kupitia hatua ya juu ya ujuzi kama vile utafutaji wa mtandao. Japokuwa mpangilio wake hutoa mwongozo wa jumla wa mtiririko ndani ya kitini hiki, kimepangwa katika hali ambayo kila kipengele kinaweza kujitegemea. Hii humwezesha mkufunzi kuchagua ni kipengele gani kitumike kulingana na walengwa wake.

Tunatumia huduma zetu tatu za WhatsApp, Youtube na Google kutambulisha huduma ya mtandao kwa watu. Na pia tunatoa utambulisho kwa mtandao, ulinzi mwamko mdogo kwenye kujifunza jinsi ya kutumia huduma nyinginezo. (mf. Facebook).

Hata hivyo, kama umejipanga kutumia kitini hiki katika maeneo tofauti, huduma za msingi utakazotaka kufund shia zitatofautiana, hii ni kulingana na walengwa wako (angalia “jinsi ya kuongoza”).

Tunatumia huduma zetu tatu za WhatsApp, Youtube na Google kutambulisha huduma ya mtandao kwa watu. Na pia tunatoa utambulisho kwa mtandao, ulinzi na gharama. Hii ni kutokana na utafiti kwa wateja unaoonyesha kwamba huduma hizi

Endapo unataka kutumia kitini hiki nchini mwako, unaweza kutumia huduma hizi kulingana na matakwa ya hadhila yako. Ukitumia ’Jinsi ya kuongoza’unaweza kupata usaidizi.

# Nini kimo ndani ya kitini hiki?

## Utangulizi wa intaneti

Watu wengi hawaelewi mtandao wa simu kupitia intaneti ni nini, hata kama walishasikia hapo awali. Tumeweka maelezo mepesi ili kujibu maswali yanayoweza kujitokeza mara kwa mara kuhusu intaneti.

## WhatsApp

Kama ilivyo katika nchi nyingi, Whatsapp imekuwa kivutio kikubwa kwa watu wa Tanzania. Na pia watu wamekuwa na uelewa mkubwa juu ya matumizi ya ujumbe mfupi. Kwa kutumia WhatsApp kama kigezo cha kuanzia itasaidia wakufunzi kueleza watu kwa kile wanachokijua, wakiwaelezea faida za mawasiliano kupitia intaneti na jinsi ya kuitumia.

## YouTube

Youtube inawezesha wanafunzi kugundua maudhui ya Intaneti. Inaruhusu wakufunzi kujenga shauku ya kuwa na mtizamo wa kimaudhui ya sauti na ya kuona, wakati huo ikitoa ujuzi wa lazima katika kutumia intaneti. Youtube inaweza isipatikane katika maeneo yote kutokana na tatizo la kuunganisha. Katika mazingira hayo, tunashauri ama kuachana na moduli ya YouTube, au kutumia utaratibu mwingine wa sauti/ au picha ambao unatumia data kidogo (mf. Utafutaji wa picha kama za Google).

## Google Search

Utafutaji wa Google unaruhusu watu kutafuta maudhui halisi katika intaneti. Hii inaruhusu mwanafunzi kuwa na uzoefu wa kina wa taarifa. Inawawezesha kufanya mazoezi katika ujuzi wao wa kutafuta. Kwa wakufunzi ambao wamewafundisha washiriki kupitia moduli ya YouTube, hii inawapa fursa kujiimarisha zaidi katika ujuzi walioupata katika YouTube.

# Nini kimo ndani ya kitini hiki?

## Wikipedia

Wikipedia ni rejea ya intaneti inayotolewa bure ili kutoa habari za uhakika kuhusu dondoo za elimu. Moduli hii inampatia mwanafunzi wigo mpana wa taarifa zinazoweza kupatikana kwenye intaneti, na katika website ya taarifa. Na pia inawafumbua akili kwamba maudhui ndani ya intaneti hubuniwa na watu wa kawaida ulimwenguni kote.

## Facebook

Facebook ni mtandao wa kijamii unaowawezesha watu kuwasiliana kwa shughuli za kibiashara, kupokea habari, mawasiliano ya familia na marafiki, au kufuatilia watu maarufu na timu za michezo. Moduli hii inaonesha wigo mpana wa yale yanayoweza kuwakilishwa na mtandao wa kijamii na kuwapatia uwelewa wa 'akaunti'na 'kugawiana'maudhui.

## Usalama na gharama

Kubaki salama na uwelewa wa gharama za kutumia mtandao wa intaneti vimeelezwa ndani ya moduli ya WhatsApp, YouTube, Google, Wikipedia na Facebook. Utafiti wetu umeonesha kwamba usalama na gharama ni mambo muhimu kwa watu wanaotumia mtandao wa intaneti nchi Tanzania, hivyo basi tuliamua kueleza haya ndani ya kila moduli ya mafunzo ya kina na kwa upande mwengine kwenye vipengele vya mafunzo ya kipimo cha kifurushi.

# Jedwali hili linatoa mwelekeo wa huduma za awali, kazi na ujuzi uliyomo kwenye mafunzo.

## Intaneti inayotembea

**WhatsApp**

Tuma na pokea ujumbe wa mtu mmoja mmoja

Anzisha na shiriki kwenye vikundi

**YouTube**

Tafuta video

**Google**

Tafuta na vinjari taarifa

**Wikipedia**

Tafuta na vinjari taarifa bure


**Facebook**

Jiunge na marafiki na familia

# Kitini hiki kinaweza kutumikaje?

Unaweza kutumia kitini hiki kwa njia tofauti kutegemea muda unaokuwa na wanafunzi.

---





**Kwa waalimu wenye dakika 2-3 tu,** wakiwa na wanafunzi wao kuna "ufupisho" wa mafunzo ulio na dakika 2- 3 za kipengele cha mafunzo ya kipimo cha kifurushi. Kila kipengele kina jumuisha mwongozo mmoja ambamo kuna miongozo sita ya kuchagua: Utangulizi kwenye intaneti, WhatsApp, YouTube, Google, Wikipedia, Facebook, Usalama na Gharama.

**Vipengele vya ufupisho vinaweza kutumika kama mapitio kwa wanafunzi waliomaliza mafunzo, lakini wangependa kurudia waliyojifunza.**

Fungua kurasa wa 8 kwa "ufupisho" wa mafunzo.

---




**Kwa wakufunzi wenye dakika 45-60 wakiwa na wanafunzi wao** kuna vipengele vinne vya kina vya mafunzo. Vipengele vya kina vya mafunzo huanzia dakika 45-60 vikiwa na utangulizi wa somo, vikifuatiwa na aina tatu za mafunzo ya huduma ya intaneti yenye urefu unaofanana. Kila moja ya vipengele vya mafunzo ya intaneti vina mwongozo mmoja: WhatsApp, YouTube na Google. Usalama na gharama vinavyojumuishwa kwa kipengele cha mafunzo.

Fungua ukurasa 30 kwa "mafunzo ya kina.

# Mafun
# kipi o
# kifuru

# nzo ya cha shi

# Namna ya kutumia mafunzo ya kipimo cha kifurushi




**Kipengele hiki ni kwa wakufunzi wenye dakika 2-3 tu kuwa** na wanafunzi wao. Inaweza kutumika kama mapitio kwa wanafunzi waliomaliza mafunzo yao, ila wangependa kurudia wa kifupi kile walichojifunza awali.

Kila kipengele kina mwongozo mmoja na kuna miongozo sita ya kuchagua: Utangulizi wa Intaneti, WhatsApp, YouTube, Google, Usalama na gharama. Kila kipengele kinalenga kutoa maelezo ya huduma na mazoezi kwenye simu.

# Kila kipengele cha kipimo cha kifurushi kinafuata muundo unaolingana:




## Ni kitu gani?

Eleza kwa kifupi kuhusu huduma. “Alama za nukuu” zinaashiria kitu gani mkufunzi angeweza kusema



## Utatumia kwa ajili gani?

Elezea kwa kifupi faida za huduma. “Alama za nukuu” zinaashiria kitu gani mkufunzi angeweza kusema



## Inafanyaje kazi?

**Fanya mazoezi!**

Tumia ‘Jinsi ya kutumia kipeperushi’ kusaidia wanafunzi kuelewa huduma kwenye simu. Unaweza kuwapatia simu yako, au wakatumia ya mwanafunzi mmojawapo




## Mazoezi!

**Fanya mazoezi**, yanayolingana na uhalisia kwa watazamaji wako

Ukurasa huu umebuniwa kumsaidia mkufunzi kujibu maswali ya jumla ambayo yangeweza kuulizwa na wanafunzi kuhusu mtandao wa simu. Inatoa maelezo mepesi ya maswali ambayo baadhi ya watu mara kadhaa wameuliza kuhusu mtandao wa simu. Ni vyema kuwa na karatasi hii kwa msaada zaidi. Utaona pia kwamba imejumuishwa ndani ya kitini hiki.

## Ni kitu gani?




**Onesha 'Kipeperushi cha Intaneti'** (uk. 115) "Intaneti ni mtandao wa mamilioni ya komputa ulimwenguni kote ambazo zimeunganishwa kupitia laini za simu, satelaiti na nyaya. Inakuwezesha kuwa na wigo mpana wa kupata taarifa na huduma na unazidi kukua kila wakati. Intaneti ni kwa kila mtu. Hakuna mipaka ya matumizi, unachohitaji ni kuwa na kompyuta, simu ya mkononi na muunganiko wa data."

## Ni Kwa matumizi gani?

"Intaneti itakusaidia kufanya mambo mengi. Kwa mfano utaweza kutuma ujumbemuziki, kuuza na kununua bidhaa, kutuma pesa. Itakusaidia kupata taarifa ya jambomichezo. Itakusaidia ata kama unatafuta ajira, huduma ya matibabu, au unahitajikujifunza ujuzi mpya."

Wakufunzi kujumuisha mifano yao binafsi jinsi gani Intaneti imewasaidia. Iwe na uhalisia kwa mwanafunzi Ijadiliwe jinsi gani itakuwa na faida kwa maisha yamwanafunzi.


## Inafanyaje kazi?

**"Kuna aina mbili za simu za mkononi unazoweza kutumia kupata intaneti:**

**1. A smartphone:** Simu hizi nikama kompyuta ndogo. Kwa kawaida unaidhibiti kwa kugusa kioo badala ya kitufe. Zinaweza kupiga picha, kucheza muziki, kucheza video na 'apps' zinazoweza huduma ya intaneti.

**2. A feature phone:** Hizi hazina mambo mengi kama zile simu za smart phone. Hazina kioo cha kugusa bali zinaweza kucheza muziki nakupiga picha. Unaweza kuingia kwenye intaneti ili kupata huduma ya mtandao.

## Gharama za data




"Ili kuingia kwenye intaneti kupitia simu yako ya mkononi unaweza kutumia kuunganishwa na data au Wi-Fi." **Onesha 'Kipeperushi cha kifurushi'** (p. 117).

"Kwa kawaida unapotumia intaneti kweye simu yako, unatumi kifurushi cha simu. Utahitaji kununua kutoka kwa wakala wa mitandao au duka linalouza vocha za simu. KKadri unavyotumia intaneti, kama vile kuangalia video au kusikiliza muziki, unatumia data zaidi, hivyo itakugharimu pesa zaidi."

## Ni kitu gani?


WhatsApp

**Onesha WhatsApp kwenye simu**

“WhatsApp ni huduma ya ujumbe, inayofanana na SMS, ambapo pia unaweza kutuma ujumbe wa sauti, picha na ujumbe wa kikundi cha watu.”

“WhatsApp inatumia kifurushi cha intaneti hivyo ni gharama nafuu kutuma ujumbe, na umbali wa unaemtumia ujumbe haubadilishi gharama. Kwa mfano, kama una jamaa yako au aliyehamia nchi nyingine, unaweza kuwatumia ujumbe wa WhatsApp, na gharama hazitatofautiana na aliyeko nyumba jirani.”

## Zana utakazo zihitaji



Smartphone




Vipeperushi vya WhatsApp

## Utaitumiaje?

“Unaweza kuitumia kuwasiliana kiurahisi kwa ndugu na marafiki.”

“Pia waweza kuitumia kwa kujiunganisha na kundi wenzio / wateja: bidhaa za matangazo, kubadilishana mawazo kushauriana, au mitihani kutoka darasani.”

Wakufunzi kujumuisha mifano yao binafsi juu ya faida ya WhatsApp na wanaitumiaje.

**Iwe mwafaka** kwa mwanafunzi: Ijadiliwe jinsi gani itakuwa na faida kwa maisha ya mwanafunzi.

## Inafanyaje kazi?

**Weka simu kwenye viganja Vya Mwanafunzi na msaidie kufuata hatua**




**Jinsi ya kutumia WhatsApp - Ujumbe1-kwa-1**
Onesha kipeperushi ukienda hatua kwa hatua jinsi ya kutuma: maandishi/ picha/ ujumbe wa sauti




**Jinsi ya kutuma ujumbe wa WhatsApp – kwa kikundi**
Onesha kipeperushi ukienda hatua kwa hatua kwa kuanzisha kikundi cha ujumbe

## Mazoezi!

**"Sasa unajua jinsi ya kutumia WhatsApp, unataka kuitumia vipi?"**

Mkufunzi: Msaidie mwanafunzi kutuma ujumbe wa WhatsApp kutumia majina yaliyomo kwenye simu zao.

**Dondoo:** "WhatsApp ina matumizi mengi. Kwa mfano, unaweza kuwapigia simu watu kupitia WhatsApp, au kuwapa ramani wenzako kuonesha mazingira uliopo kwa kutumia WhatsApp ili wafahamu ulipo."

**Elezea:** Kuna huduma za ujumbe zinazofanana na zile za WhatsApp. Na nyinginezo ni Messenger, WeChat na Viber na pia kuna nyingine nyingi.


## Ni kitu gani?

**Onesha YouTube kwenye simu**


"YouTube inakusaidia uone video, kama vile TV, ila una video zaidi kuchagua, na unaweza pia kuchagua video zipi za kuangalia na wakati gani."

"Unaiambia YouTube ni aina gani ya video unayoitafuta, na itatafuta video zote ambazo watu wameziweka kwenye YouTube, ili kupata aina ya video unazozitaka."

## Zana Utakazo zihitaji



Smartphone




Kipeperushi cha YouTube

## Utaitumiaje?

"Unaweza kuangalia video nyingi tofauti, sinema, nyimbo, habari, michezo, na mambo ya kuelimisha. Kuna mambo mengi ya'jinsi ya' mfano, jinsi ya kujifunza Lugha, jinsi ya kucheza ngoma, jinsi ya kupika chakula, jinsi ya kupachika taili kwenye baisikeli."


"Pia unaweza kutengeneza video zako mwenyewe na kuziweka kwenye YouTube."

Wakufunzi wanaweza kujumuisha mifano yao binafsi kuhusu faida za YouTube na jinsi wanavyotumia.

**Iwe mwafaka kwa mwanafunzi:** jadili jinsi utafutaji wa YouTube unavyoweza kuwa na manufaa kwenye maisha ya mwanafunzi.

## Inafanyaje kazi?

**Weka simu kiganjani mwa mwanafunzi na msaidie kufuata hatua**




**Onesha kipeperushi** na pitia hatua zote rahisi za kutafuta video (mf. tafuta 'Kanumba').

**"Kipaza sauti** kinaweza kutumika kutafuta sauti. Uhitajiki kuandika maneno yoyote."

**Onesha kwa vitendo kipaza sauti:** kiko wapi na kinatumikaje.

## Mazoezi!

**"Sasa unaifahamuYouTube, ungependa uitumie kwa ajili gani?"**

Wape wanafunzi maneno ya msingi ya kutafuta kulingana na utashi wao (jaribu kutumia utafutaji rahisi, tumia maneno 1-2 tu).

**Dondoo:** YouTube ni kubwa kwa video, lakini intaneti ni kubwa zaidi kuliko YouTube! Kunataarifa nyingi zaidi kwenye intaneti. Ukitaka kutafuta intaneti kwa ujumla, unaweza kujaribu kutumia 'Google Tafuta'.


**Elezea:** kwamba kuna huduma nyingine zinazofanana na zile za YouTube, zinazowaruhusu watu kupakia na kutazama video. Baadhi ya mifano hii ni Daily Motion na Vimeo.

## Ni kitu gani?

**Onesha Google Search kwenye simu**

"Google Tafuta inakusaidia wewe kutafuta taarifa unazozitaka. Eleza Google taarifa unazotaka kutafuta mf. 'kuna watu wangapi Keko?' na itatafuta taarifa zote ambazo watu wameweka kwenye intaneti, ili kukupatia unachotaka."

## Zana Utakazo hitaji



Smartphone




Kipeperushi cha Google

## Utaitumiaje?


"Unaweza kupata taarifa za kazi, aina za mapishi, sinema za Bongo movie, nyimbo, habari, taarifa za shule, chuo, mitihani n. k."

"Uhitaji kwenda popote kupata taarifa, zote zinapatikana kwenye intaneti ndani ya simu yako."
Mkufunzi: Toa mifano yako binafsi kwa kila dondoo, kama una muda

**Iwe mwafaka kwa mwanafunzi:** jadili jinsi Google tafuta inavyoweza kuwa na manufaa kwenye maisha ya mwanafunzi

## Inafanyaje kazi?

**Weka simu kwenye kiganja cha mwanafunzi na msaidie kufuata hatua**




**Onesha kipeperushi** na uoneshe jinsi ya kutafuta mf. tafuta alama maarufu maeneo ya karibu kama vile kanisa, au mtu maarufu kama vile mchekeshaji Joti

**Elezea** "Kipaza sauti kinaweza kutumika kutafuta sauti. Huhitaji kuandika maneno yoyote."

**Onesha kwa vitendo kipaza sauti:** kiko wapi na kinatumikaje

## Mazoezi!

**"Sasa unaifahamu Google, ungependa uitumie kwa ajili gani?"**

Wape wanafunzi maneno ya msingi ya kutafuta kulingana na utashi wao (jaribu kutumia utafutaji rahisi, tumia maneno 1-2 tu).

**Dondoo:** "Kuna taarifa nyingi na muhimu kwenye mtandao wa intaneti, kuna baadhi sio muhimu, nyingine sio za kuaminika. Ni vizuri zaidi kuangalia matokeo 2-3 ili kupata majibu yaliyo sahihi zaidi ya kile unacho kitafuta."

**Elezea:** kwamba kuna huduma nyingine zinazofanana na zile za to Google, zinazowaruhusu watu kutafuta. Baadhi ya mifano ni Yahoo na Bing

## Ni kitu gani?


**Onesha Wikipedia kwenye simu**

"Wikipedia ni rejea ya intaneti inayotolewa bure ili kutoa habari za uhakika kuhusu dondoo za elimu. Mara nyingi ndicho kitu cha kwanza kujitokeza wakati unapotafuta kwenye Google, au unaweza kuandika neno "wiki" sambamba na maneno unayoyatafuta."

"Wikipedia inaandikwa na watu wa kawaida, ulimwenguni kote. Watu hubadilisha mlengo kila baada ya saa kupita. Unaweza kuhakikisha kwamba taarifa unazozitafuta ni sahihi kwa kuangalia chini ya kila ukurasa, ambapo vianzo vya taarifa huorotheshwa.

## Zana utakazo hitaji

Smartphone




Vipeperushi Wikipedia

## Utaitumiaje?

"Unaweza kutumia Wikipedia kutafuta mambo mengi tofauti. Kwa mfano, unaweza kutafuta taarifa kuhusu michezo, muziki, historia, nchi nyingine au sayansi."


"Wikipedia inapatikana katika lugha takriban 300. Kila moja ikiandikwa na watu watumiao lugha husika, hivyo baadhi ya Wikipedia zina maandishi mengi kuliko nyingine. Kwa mfano, Wikipedia ya Kifaransa ina maandishi milioni 2, ila kuna maandishi zaidi milioni 5 kwenye Wikipedia ya Kiingereza."

**Elezea** wakufunzi kuingiza mifano yao binafsi juu ya faida za Wikipedia na wanaitumiaje.

**Ifanye ieleweke kwa wanafunzi:** jadili jinsi itakavyokuwa na faida kwa maisha ya mwanafunzi.

## Inafanyaje kazi?

**Weka simu kiganjani mwa mwanafunzi na umsaidie kufuata hatua**




**Namna na kutumia Wikipedia**
Onyesha vipeperushi hatua kwa hatua kwa kutafuta maandiko ya Wikipedia (mfano Afrika, muziki au Kombe la Dunia).

## Mazoezi!

**“Sasa unaweza kutumia Wikipedia, unataka kuitumia kwa ajili ya nini?”**

**Mkufunzi:** Toa msaada kwa wanafunzi kutafuta maandiko ya Wikipedia katika simu zao.

**Dondoo:** “Wikipedia inapatikana katika lugha takriban 300. Kila moja ikiandikwa na watu watumiao lugha husika, hivyo baadhi ya Wikipedia zina maandishi mengi kuliko nyingine. Kwa mfano, Wikipedia ya Kifaransa ina maandishi milioni 2, ila kuna maandishi zaidi milioni 5 kwenye Wikipedia ya Kiingereza.”

**Elezea:** “unaweza kugundua kuwa Wikipedia inatokea wakati ukiwa katika huduma nyingine kama Google, au Yahoo kutafuta intaneti. Mara nyingi Wikipedia ni matokeo ya kwanza wakati wa kutafuta. Mara nyingi pia unaweza kutumia Wikipedia kwanza kupata mtizamo wa mada na tena kutafuta kupitia rejea kutafuta taarifa zaidi.”


## Ni kitu gani?

**Onesha Facebook kwenye simu**


“Facebook inakuunganisha wewe na watu katika jamii dunia nzima. Unaweza kuitumia kujiunganisha katika anwani za kibiashara, kupokea habari, kuwasiliana kila mara na familia na marafiki au kuwafuatilia watu maarufu na timu za michezo” “Kwa kutumia maneno picha na video, unaweza kuwasiliana na mtu mmoja, kundi maalumu la mtu au watu duniani kote.”

“Kwa kutumia maneno, picha na video, unaweza kuwasilianana mtu mmoja, kundi maalumu la mtu au watu duniani kote.”

## Zana utakazo hitaji



Smartphone




Vipeperushi vya Facebook

## Unaweza kuitumia kufanya nini?

“Unaweza kuitumia kuendelea kuwasiliana na familia na marafiki katika mji wowote au kijiji, soma habari za nyumbani na za kimataifa na huenda na wakati kwa watu maarufu au timu za michezo.”

“Unaweza pia kutuma picha zako, video na mawazo yako kwa kila mtu, marafiki zako au marafiki zako wachache”

**Fanya uhalisia** kwa mwanafunzi: toa mifano na jadili jinsi inavyoweza kumfaidisha mwanafunzi katika maisha yake.


Kwa mfano: Kutuma picha kwa marafiki, kutafuta habari au kukuunganisha na watu wapya kwa biashara.

## Inafanyaje kazi?

**Weka simu katika mikono ya mwanafunzi na msaidie kufuata hatua**





1) Ingia kwenye Facebook





2) Fungua akaunti




3) Ongeza marafiki




4) “Kama”watu maarufu michezo na habari




5) Tuma maandishi

**Msaidie mwanafunzi** kupakua Facebook na kusajili akaunti.

**Waulize** ni nini wanataka zaidi- kwa mfano. Jambo ambalo wanahitaji kujifunza, nafasi za kazi, michezo, burudani au biashara- na kuchunga muda ni jambo muhimu kwao.

## Zoezi!

**“Sasa unafahamu kutumia Facebook, unataka kuitumia katika nini?”**

Mkufunzi: Toa msaada kwa mtumiaji kupitia mojawapo ya vipeperushi hapo juu.


**Elezea:** “Unamwongoza anaweza kuona taarifa unazoweka katika Facebook. Unaweza ukaweka posti inakonekana kwa watu wengi (kila anayetumia Facebook) au wale tu marafiki, maalumu.”

## Ni kitu gani?



"Kuna mambo makubwa unayoweza kufanya ukitumia intaneti, ila ni muhimu kukumbuka kwamba intaneti iko azi kwa kila mtu ulimwenguni na ni muhimu kuichukulia kama maisha halisi yaliyo wazi (mf. Sokoni) na kuwa salama."


## Zana Utakazo hitaji



Smartphone




Kipeperus hi cha usalama




Kipeperushi cha kuzuia na WhatsApp

## Utaitumiaje?

**Toa kielelezo cha 'Dondoo nyepesi kwa usalama wa intaneti'**

"Kama upo kwenye eneo la wazi, unapaswa

1. "Zuia' au usijibu watu usio wafahamu au wanaokusumbua"
2. Tunza taarifa zako za binafsi (mf. wewe ni nani, unaishi wapi, namba za siri)
3. Mweleze mtu unayemjua na kumwamini kwa jambo usilolielewa au unapata tatizo kwenye intaneti
4. Kuwa mpole na mwenye heshima kwa watu na usiwasumbue."

**Mkufunzi:** Toa mifano yako binafsi kwa kila sehemu, kama unao muda.

## Unawezaje kuwa salama?

### Weka simu kwenye kiganja cha mwanafunzi na umsaidie kufuata maelekezo

**Uliza ni huduma gani wanataka kujifunza ili kuwa salama kwenye (WhatsApp, YouTube, Google)?**

**WhatsApp:** "Kama kuna mtu usiye mfahamu anakutumia ujumbe ama kukusumbua kwenye WhatsApp nawe hutaki, waweza"kuzuia" hivyo hawataweza kuwasiliana nawe tena" Onesha kipeperushi cha jinsi ya "Kuzuia' na uoneshe kwa vitendo (p. 157).

---

**YouTube:** "Kama unaangalia video ya Kanumba na kuna mtu pembeni unae mdhania si mzuri au ni kikwazo kwako, unaweza kurudi kwenye ukurasa wa awali, sitisha utafutaji wako kisha endelea kutafuta video nyingine."
**Onesha kwenye You Tube** - Bonyeza kitufe cha nyuma, ondoa maneno ya msingi kwenye utafutaji kisha badili mwelekeo kwa kutumia aina nyingine ya maneno ya msingi.

---

**Google:** "Kama unatafuta taarifa za Kanumba na kuna mtu pembeni unae mdhania si mzuri au ni kikwazo kwako unaweza kurudi kwenye ukurasa wa awali, badili utafutaji wako kisha endelea kutafuta taarifa nyingine."
**Onesha kwenye Google** - Bonyeza kitufe cha kurudi nyuma ondoa maneno ya msingi kwenye kisanduku cha kutafuta na badili utafutaji kwa kutumia aina nyingine ya maneno ya msingi.

---

**Facebook:** "Kama uko katika Facebook unaweza kubadilisha anayeona maelezo yao binafsi na anayeweza."
**Onesha katika Facebook** – Onesha njia ya mkato ya siri ambapo wanaweza kurekebisha mtu wa kuona maelezo yao binafsi na kuwasiliana nao.

## Ni kitu gani?


"Unapotumia intaneti kwenye simu yako, ujue unatumia 'data'. Ina maanisha kwamba unahitaji kununua data kutoka kwenye mtandao wa simu yako. Baadhi ya vitendo kwenye intaneti vinatumia data zaidi hivyo vinagharimu zaidi."

"Unaweza kununua kifurushi cha intaneti; Kama vile kununua salio la kupiga simu na kutuma ujumbe. Kifurushi cha intaneti kinaweza kununiliwa kutoka kwa wakala wa mitandao ya simu au muuzaji wa vocha za simu atakayeweza kukutumia salio."

"Wakati mwengine vifurushi vya intaneti vinaweza kununuliwa katika vocha za vifurushi au kadi za vifurushi unavyoweza kuweka mwenyewe."

## Zana Utakazo hitaji

Smartphone




Kipeperu shi cha kipimo cha kifurushi

## Kitu gani kinatumia data?

**Kipimo cha kifurushi**

"Kiasi cha matumizi ya kifurushi yatategemea na shughuli husika. Kuangalia maandishi inatumia kifurushi kidogo, kuangalia picha unatumia zaidi, kucheza na kupakua muziki, kiambatisho na miito ya simu pia inatumia zaidi, na kupakua na kucheza video inatumia maradufu. Video ina desturi ya kutumia zaidi kifurushi kuliko matumizi mengine ya intaneti."

"Baadhi ya huduma za intaneti zinaunganishwa na shughuli zinazotumia kifurushi zaidi:

- mf. kuangalia video kwenye YouTube husababisha matumizi makubwa ya data
- mf. kutumia Google kuangalia maandishi na picha inatumia data kidogo, ila kuangalia video utatumia zaidi"

**Elezea kwamba** "Maboresho ndani ya kompyuta inatumia data na itakuwa na gharama kubwa."

## $ Unahakikishaje kipimo cha kifurushi za data?

**Weka simu kwenye viganja vya mwanafunzi na umsaidie kufuata hatua**

"Ni vizuri kuhakikisha kifurushi chako kujua kiasi ulichotumia, na tofauti ya gharama kwa kila aina ya matumizi.

Unaweza kuhakikisha kujua kiasi cha kifurushi ulichonacho, kama vile unavyohakiki dakika ngapi au maneno uliyonayo kwa kuandika kodi kwenye simu kutoka mtandaoni."

**Onesha mwanafunzi** jinsi ya kuangalia kifurushi. Hii itategemea upo nchi gani na unatumia mtandao gani. Omba msaada kwa wakala wa simu endapo utahitaji usaidizi.

**Dondoo:** "Unaweza kununua kifurushi kwa gharama tofauti kulingana na matumizi ya intaneti. Omba ushauri kwa wakala kujua ni kiasi gani mwafaka kwako kutumia."

# Mafu ya kina

# unzo

# Jinsi ya kuandaa mafunzo yako

Haya ni mapendekezo kwa ajili ya utekelezaji wa mafunzo ya kina.

## 1. Vipindi vya jinsia moja

Weka wanawake na wanaume katika vipindi tofauti vya mafunzo. Hii inatoa fursa sawa kwa uzoefu wa vitendo na kutoa nafasi ya kujadili vikwazo kijinsia bila kificho

## 2. Mazoezi ya kundi ndogo

Weka wanafunzi katika makundi madogo madogo Yasiyozidi watu sita. Weka mkufunzi mmoja kusimamia kila kundi. Hii itawawezesha wanafunzi kupata uzoefu kwa vitendo nakuruhusu elimu iliyonyooka

## 3. Makundi kulingana na ujuzi

Weka wanafunzi katika makundi wenye akili na ujuzi unaofanana. Ni muhimu kuwa na watu wenye ujuzi unaofanana katika kundi moja, ili wajiamini na kuwa huru. Kuwa huru kuhamisha wanafunzi katika makundi tofauti, baada ya mafunzo kuanza, iwapo itafahamika kuwa wanafunzi hawako katika kiwango sawa cha ufahamu katika makundi yao.

## 4. Matumizi ya vifaa

Endapo watu hawana simu zao binafsi za mkononi, wape simu zinazofanana zenye data za kutosha. Hakikisha simu zote zinafanana (kwa mfano zina mfumo sawa wa kiutendaji). Hii inamsaidia kila mmoja kwenda hatua kwa hatua wakati wa mafunzo na kuwa makini zaidi katika matumizi binafsi ya data na kubadilishana taarifa binafsi. Ikiwezekana tunashauri hakutakiwi kuwa na zaidi ya watu watatu kwenye kifaa kimoja.

# Dondoo kwa wakufunzi

## Anza na za msingi

Hata kama wanafunzi watakuwa na uzoefu na huduma za intaneti, wanaweza kuwa na upungufu.

## Iwe nyepesi

Tumia maelezo ambayo si ya kitaalamu

## Onesha uhalisia

Tumia mifano binafsi kuvuta hisia za wanafunzi

## Himiza vitendo

Jielekeze katika kumuonesha mwanafunzi

## Shukuru wanafunzi

Wanafunzi wanafunzi wenye hamasa chanya vyeti. Kama ikiwezekana

## Zungumza na wanafunzi

Himiza mawasiliano pande zote kati ya wanafunzi na mwalimu

# Jinsi ya kutumia mafunzo ya kina

**Haya ni mafunzo ya kina kuongoza wakufunzi ambao wanakuwa na wanafunzi kwa dakika 45-60.**

Mafunzo haya yanajumuisha vipengele vinne ndani ya dakika 45-60. Yanaanza na utambulisho na kufuatiwa na vipegele vitano vinavyogusa mada moja katika: WhatsApp, YouTube na Google, Wikipedia na Facebook. Usalama na gharama vimewekwa katika kila kipengele.

Hata hivyo, mafunzo yamewekwa katika mfumo ambao kila kipengele kinaweza kusimama chenyewe. Hii ina maana ya kwamba unaweza kuchangua kipengele cha mafunzo unachotaka kutumia wewe na wanafunzi wako, kwa kuzingatia kipi kilicho bora kwao. Kama huwezi kutumia Youtube katika eneo lako kutokana na tatizo la kimtandao, unaweza kuhairisha moduli hiyo ns kutumia ile ya kuona moja kwa moja ambayo inahitaji data kidogo.

## Mafunzo ya kina yana aina kuu nne za vitendo:

**Maelezo.** Maelezo mafupi kuelezea faida za huduma

**Maelezo ya vitendo kwenye simu**

**Majadiliano.** Maelezo ya vitendo kwenye simu

**Rejea.** Kusisitiza masomo kila moduli

# Orodha ya vipengele katika Mafunzo

Kabla ya kila kipengele cha mafunzo, hakikisha unajipatia muda wa kutosha wamaandalizi. Hakikisha unapata muda wa kutosha kuandaa simu za mkononi. Hii inaweza kuchukua muda mrefu zaidi ya unavyofikiria!

- Angalia kama una zana zote zitakazohitajika wakati wa Kipindi (angalia zana zinazohitajika katika ukurasa wa mapitio Katika kila moduli)
- Hakikisha simu zote zimechajiwa
- Pakua na weka sawa huduma zote ulizopanga kutumia katika simu.


  *Kitini hiki hakina moduli ya jinsi ya kupakua apps. Hii ni kwasababu kimetengenezwa katika mtindo unaohotaji akaunti ya email ambao wanafunzi wapya au wanaoanza hawatakuwa nayo. Hata hivyo simu nyingi za sasa za Android zina Youtube na Google zilizounganishwa kabla. Kama unahitaji msaada wa jinsi ya kupakua WhatsApp, na Facebook au Wikipedia, tafuta mwongozo wa kukusaidia hapa.*
- Hakikisha namba zote za simu utakazotumia zimeunganishwa katika simu zitakazotumika wakati wa mafunzo
- Ondoa taarifa binafsi (mfano picha, ujumbe n. k) kabla ya kukabidhi simu kwa washiriki
- Elewa yaliyomo katika mafunzo
- Weka sawa intaneti katika simu zote zilizounganishwa na mtoa huduma ya mtandao (kumbuka hii inaweza kuchukua siku kadhaa)
- Ipe simu yako jina, weka lebo nyuma ya kila simu kwa jina lake na namba yake ya simu ili ujue wakati wa mafunzo
- Angalia kuunganishwa kwake kama inatumia Mi-Fi/Wi-Fi, Aangalia kama zote zinafanya kazi na kama ziko hewani katika simu
- Jaza data ya intaneti katika simu zote

# MODULI 1 UTANGULIZI

# LI 1 – GULIZI

## Malengo ya mafunzo


- Kuelewa sababu ya mafunzo na kujua nani yuko ndani ya chumba
- Jenga tabia: hakikisha mwanafunzi anakuwa salama, kujiamini na kuhamasishwa kujifunza intaneti ya simu na kujua sheria zake
- Kufahamu faida za msingi za kutumia intaneti katika maisha yao




**Muda wa kipindi:**
Dakika 45-60

**Dondoo:** Andaa ukurasa wa nyumbani wa intaneti kupitia Google katika kifaa kinachotuma kwa kuonesha sehemu maarufu za kawaida. Hii itamfurahisha mwanafunzi na kumvutia kama sehemu yake ya kwanza ya uzoefu. Kutengeneza ukurasa wa nyumbani, fungua sehemu ya kutafutia, nenda katika mtandao unaotaka kutumia kama ukurasa wako wa nyumbani. Fungua orodha ya chaguo, nenda kwenye settings, tumia ukurasa huo kama ukurasa wako wa nyumbani.

## Zana utakazohitaji




Simu za Smartphone





Kipeperushi binafsi x 3


Kwa wanaume onesha mwanaume, kwa wanawake onesha mwanamke




Aina za nembo








Kalamu, karatasi, gundi ya ukutani na mpira mdogo.




Vipeperushi vya mkononi




Sheria za msingi



Zawadi ndogo ndogo


# Anza na michezo ya kuvutia



### Mchezo wa utangulizi

- Chukua mpira mdogo katika kiganja chako na jitambulishe rasmi kama mkufunzi: sema jina lako, maelezo yako ya nyuma, na kwanini huko hapa
- Rusha mpira kwa mmoja wa wanafunzi wako, na mwambie asimame na kujitambulisha katika kundi. Mara atakapomaliza, mwambie arushe kwa mwingine
- Mchezo unakwisha wakati kila mmoja katika chumba akishika mpira na kujitambulisha


# Utangulizi wa mafunzo




### Eleza malengo ya mafunzo:

- "Tuko hapa kujifunza juu ya intaneti ya simu ni nini, jinsi ya kutumia na unaweza kufanyia nini."
- **Jadili** sheria zake
- **Elezea** ni nini kitajadiliwa katika mafunzo. Kwa mfano jinsi ya kutumia WhatsApp, YouTube, Google, Wikipedia and Facebook kwa kila moja
- **Elezea** "Utatanguliza intaneti katika smartphones"
- **Elezea** wajibu wa wakufunzi: "Kama wakufunzi tuko hapa kukusaidia kujifunza na kukuwezesha"
- **Elezea** "Leo ni wewe tu; Hakuna jibu baya au zuri au maswali. Sio mtihani tunataka kukusaidia kujifunza!"

# Utengenezaji wa makundi madogo



**Weka wanafunzi wako katika makundi madogo**
(Sio zaidi ya watu sita kila kundi).

Unganisha makundi hayo kwa mstari katikati ukichora kwenye sakafu:




- **Wambie** wanafunzi kila mmoja asimame katika kiduara ambacho kinawakilisha matumizi ya intaneti ya simu ya mkononi
- **Weka wanafunzi katika makundi** yasiyozidi sita kulingana na pale waliposimama- kila mkufunzi katika chumba atahusika na kundi moja
- **Elezea** kwamba makundi haya yatatumika muda wote wa mafunzo.

**Dondoo:** Ni muhimu sana kwamba, wanafunzi wawe na kiwango sawa cha uelewa katika kundi lao. Watajiamini na kuwa huru. Kuwa huru kuhamisha wanafunzi kutoka kundi moja hadi jingine baada ya mafunzo kuanza, kama itatokea hawako katika kiwango sawa cha ujuzi.

## Utangulizi makundi madogo:

- **Wambie** kila mmoja kujieleza anatokea wapi na anapendelea nini.
- **Wambie** wanafunzi kuandika majina katika ufito wa gundi na aubandike kifuani mwake.
- **Weka kusudio katika mafunzo:** Uliza “Unataka kujifunza nini?”
- **Andika** kila kusudio la mwanafunzi katika mafunzo kwenye karatasi na badika bandika ukutani.


# Elezea faida za intaneti

**Elezea kwamba mkufunzi atauliza maswali na wanafunzi watanyoosha mikono kujibu:**

- “Nani hapa amewahi kutumia intaneti kwenye simu yake kabla?”
- “Kuna anayeweza kusimama na kutueleza intaneti ni nini?”

**Elezea intaneti ni nini na ilitokea wapi**

- **Elezea** “Mtoa huduma wa simu yako ya mkononi anaweza kukuunganisha kupitia simu yako”




## Onesha ‘kipeperushi cha intaneti’

- **Elezea** “Intaneti ni mtandao unaoruhusu kompyuta na baadhi ya simu za mkononi kutuma na kupokea taarifa duniani kote. Ni kama maktaba ya taarifa, ambazo watu wanahitaji kuzipata, kuzitumia na kuwa nazo”




## Onesha ‘Vipeperushi binafsi’

Hivi ni vipeperushi vinamsaidia mwanafunzi kuonesha umuhimu wa matumizi ya simu ya mkononi

- **Elezea** “Intaneti inaweza kukusaidia kukuza biashara yako, kuendeleza ujuzi wako, kujali familia yako na mengi zaidi!”

# Elezea faida ya Intaneti

## Leta faida za Intaneti katika maisha!

**Elezea Historia yako** jinsi intaneti inavyokusaidia (Mkufunzi), marafiki zako na familia yako au jamii yako. Baadhi ya mifano inatakiwa kuhusishwa:

- Kuunganisha watu katika **WhatsApp** - kupata habari kutoka kwa marafiki na familia, tangaza biashara yako na mtandao wako n. k.
- Jifunze na endeleza ujuzi wako na pata burudani katika **YouTube** Mfano 'Jinsi ya' Video za kucheza, Maelezo ya jinsi ya kupika, au jinsi ya kubadilisha taili katika baiskeli.
- Tafuta taarifa muhimu katika **Google** za kukusaidia katika maisha yako, kazi za shule, biashara n. k

---


## Fanya intaneti kuwa halisi kwa wanafunzi

Jadili na wanafunzi namna ambavyo intaneti itawasaidia:

- **Uliza** "Umejifunza nini katika matumizi ya intaneti ambacho kitakusaidia?" Wape mapendekezo
- **Uliza** "Ni nini ambacho kimekufurahisha na unataka kujifunza juu yake?"

**Dondo:** Oanisha mijadala na vitendo katika mafunzo ili kufahamu tena jinsi intaneti inavyoweza kuwasaidia katika maisha yao. Hii itasaidia kuongeza uhalisia wa mafunzo na kuwavutia zaidi.

# Gawa smartphones



**Wagawie smartphones** (hakikisha wasiwe zaidi watatu katika simu moja)

- **Onesha kwa vitendo** Jinsi ya 'kugusa' (gusa nembo katika kioo), 'pangusa' (sogeza vidole kulia au kushoto, vuta, 'vuta zoom' (Sogeza vidole viwili kwa pamoja kwenye kioo)
- **Wambie** wanafunzi kushika simu zao tena. Wambie wajaribu tena kucheza nazo kugusa kupangusa na kuvuta picha
- **Wambie** wanafunzi kugusa kwenye nembo kwenye kioo na kuona kitakachotokea



**Dondoo:** Onesha wanafunzi ambao mishipa yao haina mazoea na simu mahala ilipo nembo ya "Camera" na kuwahimiza kupiga picha kutumia simu. Hii itawasaidia kupata burudani na kuwa na uhuru zaidi katika kugusa gusa simu.

## Wambie wanafunzi wao kupiga picha za pamoja (Picha ya kundi kwa kutumia simu!)

**Wambie** wanafunzi waoneshe picha kwa mkufunzi na wakufunzi wengine

## Jadili na wanafunzi wako walichoona katika simu


- **Uliza** "Ni wapi inaonesha nguvu ya beteri?"
- **Uliza** "Ni wapi inaonesha ishara ya simu?"

## Jadili na wanafunzi kwanini ni 'smart' phone

- **Uliza** "Kitu gani kinafanya kuwa 'smart'?"

**Dondoo:** Wape muda wa kutosha wanafunzi wako kuchezea simu na kugundua vitu.

## Kitendo: Cheza ‘Tafuta nembo ’ ya mchezo



- **Bonyeza** kila nembo ya simu kila kimoja kwa wakati wake
- **Uliza** “Nembo hii iko wapi katika simu na ni nini?”
- **Elezea** kwa wanafunzi kila nembo maana yake endapo wanahitaji msaada
- **Toa zawadi ndogo** (mfano pipi) kwa majibu sahihi na weka nembo ukutani baadaye kuwakumbusha wanafunzi wako wanachokijua

# Kitendo: Ingia kwenye Intaneti



- **Waambie** wanafunzi wako kutafuta "mpira" nembo ya intaneti katika vioo vya simu zao na kubonyeza. (intaneti itafunguka kwenye mtandao uliochagua. Angalia, maelezo p.20). Kumbuka kwamba simu tofauti zina tofauti katika utafutaji (Angalia hapo chini)
- **Elezea:** "Kwa sasa nyote mko katika intaneti. Hivyo ndivyo ilivyo rahisi! Hongera!"
- **Wape** muda wanafunzi wako kufikiria na kujadili wanachokiona


**Dondoo:** Kuna 'browsers' tofauti katika matumizi ya intaneti. Baadhi yake ambazo ni maarufu sana ni hizi zilizooneshwa hapa nchini. Inategemea na simu unayotumia. Unaweza kutumia kati ya hizi na si zilizooneshwa hapa juu.

# Moduli WhatsApp

# i 2 - sApp


## Malengo ya kujifunza

- Mwanafunzi ajifunze kuwasiliana kwenye WhatsApp
- Wanafunzi wavutiwe na kuhamasika juu ya zana





**Muda wa kipindi:**
Dakika 45-60

## Zana utakazohitaji:



Kalamu, karatasi na Gundi yakaratasi




Simu za Smartphone




Zawadi ndogo




Vipeperus hi vya WhatsApp x3




vIpeperushi vya mkononi




Kipeperushi cha gharama




Dondoo za usalama



Aina za nembo

# Tambulisha WhatsApp

WhatsApp

## Onesha wanafunzi nembo ya WhatsApp na waambie waitafute katika simu zao.

**Uliza** "Kuna anayejua hii ni nini?" "Ni ya nini?"

## Toa maelezo mafupi kuhusu WhatsApp:

- "WhatsApp inarahisisha mawasiliano ya kuchati na watu, familia, marafiki na ndugu"
- "WhatsApp ni huduma ya ujumbe, kama vile SMS, lakini pia unaweza kutuma ujumbe wa sauti, picha, video, na hata pia ujumbe wa makundi ya watu
- WhatsApp hutumia data ya intaneti badala ya salio la simu. Hii ina maana kuwa inaweza kuwa rahisi zaidi kutuma ujumbe na umbali wa mtu unayemtumia hauingii katika gharama."

## Huleta manufaa katika maisha!

- Hadithia historia yako jinsi unavyofaidika na WhatsApp katika maisha yako (mkufunzi), rafiki yako na familia. Kwa mfano: baadhi ya mifano ihusishe:
- Kuunganisha na watu wa makundi makubwa kibiashara/ ndugu/ jamaa, uliosoma nao/ Marafiki/ familia, kutangaza bidhaa, kubadilishana ushauri, kujadili muktasari au majukumu kutoka darasani na kupeana habari
- Toa mfano bayana au historia ya jinsi WhatsApp inavyoweza kutumika

## Ifanye WhatsApp kuwa halisia kwa wanafunzi

Jadili na wanafunzi jinsi WhatsApp inavyoweza kuwafaidisha katika maisha yao

- **Uliza** "Ungetaka kutumia WhatsApp kwaajili ya nini katika maisha yako?" Wape mapendekezo kutokana na wakipendacho
- **Uliza** "Kitu gani unapendelea na kimekufurahisha kuhusu WhatsApp?"

**Kumbuka:** Husisha mjadala na vitendo katika mafunzo kurejea jinsi jinsi intaneti inavyoweza kusaidia au kutumika kwa maisha ya wanafunzi. Hii itasaidia kujenga uhalisia wa mafunzo na kuwavutia wanafunzi.

# Kitendo: Ujumbe wa mmoja mmoja

## Fanya mazoezi!

**Elezea** "Sasa unakwenda kujaribu kutumia WhatsApp katika simu."




## Onesha 'namna ya kutumia WhatsApp: kipeperushi cha ujumbe wa mmoja mmoja

- **Elezea** "Kipeperushi hiki kinaonesha hatua ya kutuma ujumbe wa mtu mmoja mmoja kwenye WhatsApp"
- Wapitishe wanafunzi wako katika hatua kwenye simu zao zilizounganishwa na waeleze kwamba unaweza kutuma ujumbe umbo au ujumbe sauti

Wambie wajaribu kutumiana ujumbe wenyewe kwa wenyewe katika simu.

**1. Tuma maandishi yenye ujumbe wa salaam:**

- Bonyeza nembo ya WhatsApp
- **Elezea** wapi pa kuipata na onesha jinsi ya kuitumia
- **Waambie** wanafunzi watumiane ujumbe wa salamu wao kwa wao

**2. Tuma picha ya kujipiga ya kundi lao:**

- Bonyeza nembo ya kamera kwenye WhatsApp.
- **Elezea** jinsi ya kupata kamera, mahali inapatikana na jinsi ya kuitumia
- **Wambie** wanafunzi watumiane picha hizo

**3. Tuma ujumbe wa sauti wa salamu:**

- Bonyeza nembo ya kipaza sauti kwenye WhatsApp
- Elezea wapi pa kuipata na onesha jinsi ya kuitumia
- Waambie wanafunzi watumiane ujumbe wa sauti wa salamu wao kwa wao

- **Elezea** "Wakati unapotuma ujumbe wa WhatsApp unaweza kuona kama umefika katika simu zao na kama wameusoma". A) tuma = alama 1 ya kijivu B) Umefika = alama 2 za kijivu C) Soma = alama 2 za bluu
- **Uliza** "Unaweza kufikiria baadhi ya mifano ya wakati wa kutuma ujumbe wa sauti, au picha kuliko ujumbe?"

# Kitendo: Ujumbe wa kundi

**Elezea** “Sasa unakwenda kujaribu kutuma ‘kuchati kwa kundi’.”

**Elezea;** Elezea kuchati kwa kundi kwenye “WhatsApp, zaidi ya mtu mmoja inakuwa mazungumzo ya kikundi.”




## Onesha ‘Namna ya kutumia WhatsApp: Kipeperushi cha ‘ujumbe wa kikundi’

- **Elezea** “Kipeperushi hiki kinaonesha hatua za awali za kuunda kundi la WhatsApp”
- **Onesha kwa vitendo jinsi ya kuunda** kundi la WhatsApp na kuwaongeza wanafunzi wako, simu zilizounganishwa kwa wote kuwa katika kundi moja la WhatsApp (Tuma namba za unaowaongeza katika simu zilizounganishwa)
- **Tuma maandishi au ujumbe wa sauti kwa kundi la**’ WhatsApp la wanafunzi ili watumiane picha za kujipiga napochati kama kundi
- **Uliza** “Unaweza kufikiria baadhi ya mifano ya wakati wa kutuma ujumbe wa kundi kuliko ujumbe wa mmoja mmoja?”

**Dondoo:** Acha kundi la WhatsApp la wanafunzi likiwa hewani kwa mafunzo yaliyosalia na waambie wanafunzi kuendelea kuchati. Mfano kubadilishana mawazo, hisia, picha yoyote na mrejesho katika kuchati kwenye kundi.

# Matumizi binafsi

**Jadili** na wanafunzi wako namna ambavyo wanaweza kufaidika na WhatsApp katika maisha yao

- **Uliza** “Sasa unafahamu namna ya kutumia WhatsApp, Unataka kuitumia wapi katika maisha yako?” Wape mapendekezo kulingana na wanachokipendelea
- **Uliza** “Unapendelea nini zaidi cha kukuvutia kufanya hivyo. Sasa unajifunza namna ya kutumia WhatsApp?”

# Usalama

**Uliza** "Nini maana ya usalama?"

**Uliza:** wanafunzi wako kufikiria endapo wako katika sehemu ya umati, mfano sokoni. Wambie kujadili watafanyaje kuzingatia usalama katika eneo hili. Waulize maswali yafuatayo na majibu:

| Swali | Jibu sahihi |
|---|---|
| Unafanya nini kama mtu usiyemfahamau anakubughudhi? | Unamuepuka au unamnyamazia. Kuwa-makini mara nyingi wanachosema ni tofauti na wanavyoonekana. |
| Utafanya nini endapo mtu usiyemfahamu au kumuamini anakuuliza taarifa zako binafsi? | Usitoe taarifa zako kwa mtu usiyemfahamu au kumwamini kwasababu anaweza kuzitumia vibaya. |
| Unafanyaje kama huna uhakika juu ya jambo unaloliona au ulilozoea kuliona? | Mwambie mtu unayemfahamu na amini juu ya kile kilichotokea |
| Unawachukuliaje watu unaokutana nao? | Kuwa mwema na mtiifu kwa watu |


**Elezea:** "Ni muhimu kukumbuka kwamba intaneti ni sehemu ya wengi na ni muhimu kuchukulia hali hiyo kama mahala pa wengi ili kuwa na usalama."

# Usalama




## Mpe mwanafunzi wako kitini cha Wdondoo za usalama'

- **Jadili** na wanafunzi wako maana ya dondoo hizo katika matumizi ya intaneti
- **Lete dondoo katika maisha kwa kutumia** mifano halisi kwa wanafunzi wako. Kwa mfano wanawake wanaweza kuchangia sana kuzuia usumbufu





## Usalama wa WhatsApp

- **Uliza** "kama mtu ambaye haumfahamu anajaribu kukutumia ujumbe ama kukubughudhi katika Whatsapp na haufurahii hayo, utafanya nini?"
- **Elezea** "Kwenye WhatsApp unaweza kuwazuia na hawawezi kuwasiliana na wewe tena katika namba hiyo"
- **Onesha kipeperushi cha mchakato** onesha kipeperushi cha mchakato na kwa vitendo onyesha jinsi ya kumzuia mtu kwenye WhatsApp

# $ Gharama

**Elezea:** "Sasa unajua kutumia WhatsApp, na inaweza kutumika katika nini, ebu tuzungumzie juu ya gharama za matumizi! Kutumia intaneti katika simu yako lazima ununue data kutoka kwa mtoa huduma wa mtandao."

**Elezea:** "Gharama za kila ujumbe ni bei rahisi zaidi kuliko SMS. Hata kama unayewasiliana naye yuko mbali (hata kama ni nchi nyingine) haibadilishi gharama. Inaweza kuwa taifa jingine au mlango unaofuata kutoka nyumbani kwako."




## Onesha 'Kipeperushi cha gharama'

- **Elezea** "vitendo tofauti hutumia kiasi tofauti cha data. Ukiangalia maandishi hutumia kidogo, hutumia zaidi. Kucheza na kupakua muziki hutumia kiasi kikubwa zaidi na kucheza hutumia zaidi"
- **Elezea** "Baadhi ya huduma kucheza video za intaneti zimeunganishwa katika matukio yanayotumia data zaidi"
- **Uliza** "WhatsApp iko wapi katika Kipeperushi?" na ina maanisha nini kwa kiwango kipi cha gharama?"
- **Uliza** "Kipi kinafanya gharama kuongezeka? Jibu "Video"
- **Uliza** "Kipi kinafanya gharama kupungua?" Jibu "Kutumia maandishi"

# $ Gharama

## Angalia data

- **Uliza:** "Kwanini ni muhimu kuangalia kiasi cha data ulizotumia?"
- **Jibu:** "Kufahamu ni kiasi gani cha data yako ulichotumia na inakugharimu kiasi gani kwa matukio yote"
- **Elezea:** "Unaweza kuangalia ni kiasi gani cha data unacho, kama vile unavyoangalia dakika au maandishi uliyonayo ; kwa kuandika neno la siri katika simu yako katika mtandao wa simu ya mkononi"
- **Elezea:** "Unaweza kununua za gharama tofauti kulingana na matumizi fulani la Intaneti. Pata ushauri kutoka kwa wakala wako kufahamu ni kiasi gani kinafaa kwako."
- **Elezea:** "Kama unatumia intaneti kupitia Wi-Fi, hautatumia kifurushi chako cha data. Wakala wako atakusaidia kutafuta Wi-Fi iliyoko karibu. Hata hivyo ya ukanda wa karibu inaweza kuwa mbali pia kuifikia
- **Waoneshe** wanafunzi wako namna ya kuangalia data zao

**Dondoo:** Angalia jinsi ulivyothaminisha data kulingana na nchi ulioko na ni mtandao gani katika simu unafanya kazi. Muuliza wakala wako kama unahitaji msaada wa jinsi ya kuangalia data

# Rejea



## Cheza mchezo wa nembo ya WhatsApp

- **Bonyeza** kila nembo ya WhatsApp, kila moja kwa wakati wake
- **Uliza** "Hiki kiko wapi katika simu na ni nini?"
- **Elezea** kwa wanafunzi wako kila nembo maana yake, endapo wanahitaji msaada
- **Toa zawadi ndogo** (mfano pipi) kwa majibu sahihi na weka nembo ukutani baadaye kuwakumbusha wanafunzi wako wanachokijua

**Elezea:** Kwamba kuna huduma za ujumbe zinazofanana kwenye WhatsApp. Hizi ni pamoja na Telegram, Line, Viber, Hike or Facebook Messenger.

---

**Dondoo:** "Maombi mengi na huduma katika intaneti yanatumia nembo zinazofanana na maneno. Wakati unatumia intaneti angalia kwa makini nembo hizi, ili ukiziona wakati mwingine ufahamu zina maanisha nini."

---

## Rejea WhatsApp

- **Jadili na wanafunzi wako ni nini walichojifunza kuhusu matumizi ya WhatsApp**
- "Nini umejifunza juu ya matumizi ya WhatsApp?", "Kwanini unaitumia?"
- "Ina tofauti gani na SMS?", "Kitu gani unaweza kukifanya na WatsApp ila usikifanye kwa SMS?'
- Una swali lolote juu ya WhatsApp?"
- "Unataka kutumia WhatsApp sehemu gani katika maisha yako?", "Ni kitu gani kinakuhamasisha kuitumia?"

**Dondoo:** Pitia rejea kama chemsha bongo na toa zawadi (mfano pipi) kwa wanafunzui kucheza.

# Rejea

**Dondoo:** Kama wanafunzi watahitaji kutumia intaneti na WhatsApp katika simu zao, Wape muda fulani kufanya majaribio juu ya walichojifunzana kuwapa msaada na hamasa

## Kwenda kiwango kingine

Kama umefikia mwisho wa kipengele na badou na muwa wa ziada:

- **Uliza**: Una maswali zaid juu ya chochote tulichogusia wakati wa kipindi?
- **Uliza**: Nini kingine ungependa kufahamu juu ya intaneti ya simu?

---

Viashiria vingine zaidi vya WhatsApp ambavyo unaweza kuvijadili na wanafunzi wako ni pamoja na:


- **Pakia picha** kutoka kwenye hazina yako simu kwenda kwenye mazungumzo yako ya WhatsApp
- **Sema mahala ulipo katika** WhatsApp ili marafiki na familia wajue ulipo
- **Unda ukurasa wa WhatsApp** wa maelezo binafsi ikiwamo muundo wa siri
- **Pakua apps** kutoka kwenye hidahi yake (Utahitaji kuhusisha barua pepe, kwasababu kuwa na barua pepe ni muhimu katika kupahua apps)

# Moduli 3 YouTube

# l 3 -
# be

## Malengo ya kujifunza

- Wanafunzi kufahamu jinsi ya kutumia YouTube, kupata video na muziki
- Wanafunzi kuelewa upana wa maudhui yaliyomo na kuhamasika na kuvutiwa na uhalisia wa yaliyomo katika YouTube









**Muda wa kipindi:**
Dakika 45-60

**Kumbuka:** YouTube inaweza isipatikane katika maeneo yote kutokana na tatizo la uunganishwaji. Kwa tatizo kama hilo, tunapendekeza mwanafunzi asifanye moduli ya youtube ama aifanye nyingine ya audio au visual ambayo inahitaji data kidogo.

audio au visual ambayo inahitaji data kidogo zaidi ili ifanye kazi. Mbadala wake, unaweza kubadili muundo wa akaunti ya YouTubes kwenye simu ili icheze video kwa kutumia bandwidth ya kiwango cha chini. Zaidi ya hapo unaweza kupakua video za YouTube na kuzicheza kwa kubonyeza nembo ya video.

## Zana utakazohitaji:

| | | | |
|---|---|---|---|
|  Kalamu, Karatasi na gundi ya karatasi |  Simu za Smartphone |  Zawadi ndogo |   Kipeperushi cha YouTube x1 |
|   Vipeperushi vya mkononi |   Kipeperushi cha gharama |   Dondoo za usalama |  Aina za nembo |

# Tambulisha YouTube

## Onesha wanafunzi nembo ya YouTube na waambie waitafute katika simu zao

**Uliza** "Kuna anayejua hii ni nini?" "Ni ya nini?"

## Toa maelezo mafupi juu ya YouTube

- "YouTube inakusaidia kuona video, lakini unapata video zaidi za kuchagua. Unaweza kuchagua video za kuangalia na wakati gani."
- "Unaiambia aina ya video unazohitaji kutafuta na itatafuta katika video zote ambazo watu wameziingiza katika YouTube. Kutafuta aina zote za ambazo unahitaji."
- "Unaweza kuangalia video nyingi tofauti, nyimbo, habari, michezo, ratiba na elimu. Kuna aina nyingi za 'Namna ya' Kwa mfano nama ya kujifunza lugha, namna ya kucheza dansi, maelekezo, namna ya kubadilisha taili katika basikeli na mengineyo."
- "Unaweza pia kutengeneza video zako binafsi na kuwatumia wengine katiks YouTube."

## Huleta manufaa katika maisha!

Hadithia historia yako jinsi unavyofaidika na YouTube katika maisha yako (mkufunzi), rafiki yako na familia. Kwa mfano: baadhi ya mifano ihusishe:

- Angalia muziki nyimbo, jifunze ujuzi mpya, boresha ujuzi, tengeneza video zako
- Toa mifano halisi au historia jinsi YouTube inavyoweza kutumika

## Ifanye YouTube kuwa halisia kwa wanafunzi

Jadili na wanafunzi wako jinsi YouTube inavyoweza kuwafaidisha katika maisha yao:


- **Uliza** "Ungetaka kutumia YouTube kwaajili ya nini katika maisha yako." Wape mapendekezo kutokana na wakipendacho
- **Uliza** "Kitu gani unapendelea zaidi na kimekufurahisha?"

**Kumbuka:** Husisha mjadala na vitendo katika mafunzo kurejea jinsi YouTube inavyoweza kusaidia au kutumika kwa maisha ya wanafunzi. Hii itasaidia kujenga uhalisia wa mafunzo na kuwavutia wanafunzi.

# Kitendo: Matumizi ya awali ya YouTube


## Fanya mazoezi!

**Elezea** “Sasa unakwenda kujaribu kutumia YouTube katika simu,”




## Onesha namna ya kutumia kipeperushi cha YouTube’

- **Elezea:** “Hiki kipeperushi kinaonesha hatua za kutumia YouTube kutafuta video”
- Wapitishe wanafunzi wako katika hatua kutumia simu zao zilizounganishwa kwa kuwaonesha njia nyepesi ya utafutaji wa YouTube




## Onesha ukurasa kwa video maarufu

- **Elezea** kile wanafunzi wako wanachokiangalia:
- “Picha ya juu ni video: Unaweza kubonyeza icheze au kuzuia”
- “Huu ni muda ambao video hii imetazamwa na watu katika YouTube na inaweza kukuonesha ni jinsi gani ilivyo maarufu”
- “Unaweza ku ‘like’ au usi ‘like’ kwa kubonyeza nembo ya kidole. Namba inayofuata inaonesha ni watu wangapi wame ‘like’ au hawaja ‘like’”
- “Hizi ni muunganiko katika video nyingine ambazo unaweza kuziona na zinafanana”
- “Unaposogeza kuelekea chini utaona kiboksi cha maoni ambapo watu wameandika maoni kuhusu video hiyo”

**Uliza** “Una swali lolote kuhusu unachokiangalia hapa?”

# Kitendo: Matumizi ya awali ya YouTube

## Nyanyua juu nembo ya kipaza sauti cha YouTube

- **Elezea**. "Kipaza sauti kinaweza kutumika, hivyo hutakiwi kuandika maandishi yoyote. Wakati ambao huwezi kutaja au kuandika maneno unayohitaji kutafuta, unaweza kuiambia YouTube maneno unayotaka kutafuta"
- **Onesha kwa vitendo wapi pa kutafuta:** "Bonyeza katika kiboksi cha kutafuta na kipaza sauti kitatokea kulia"
- **Onesha kwa vitendo namna ya kutumia:** "Sogeza nembo ya kipaza sauti na zungumza kwa sauti, kwa ufasaha na taratibu"
- **Waambie wanafunzi** wako kutafuta chochote kutumia kipaza sauti

## Waambie wanafunzi wako kutafuta video katika mazoezi yafuatayo:

1. Andika jina la wimbo maarufu wa kawaida katika kiboksi cha kutafutia cha YouTube, na cheza huo wimbo
2. Andika sehemu maarufu ya kawaida katika kiboksi cha kutafutia na icheze
3. Wambie neno moja wanafunzi wako walindike katika kiboksi cha kutafutia, hii ni halisi kwao kwa mfano, 'maelekezo', 'kazi', 'kilimo', na cheza kitakachopatikana

## Kitendo: Kutafuta maneno mawili

**Elezea:** “Sasa tunakwenda kujaribu kwa undani utafutaji wa maneno- Hii inaweza kusaidia zaidi kutafuta video unazotaka”

**Wambie** wanafunzi wako wafanye mazoezi ya kutafuta video kwa kuweka muungano wa maneno mawili au matatu katika kiboksi cha YouTube cha kutafutia. Wanaweza kufanya hivi kwa kutumia kipaza sauti au kuandika maandishi. Wape maneno tofauti wayaunganishe, kwa kuzingatia walichokitafuta hapo awali. Kwa Mfano:

- ‘Africa’, ‘new’, music’
- ‘Premier League’, ‘best’, ‘goals’

**Dondoo:** Wape muda zaidi wanafunzi wako kupitia matokeo na maneno tofauti.

## Kitendo: Utafutaji binafsi

**Jadili** na wanafunzi namna ambavyo YouTube inaweza kuwasaidia katika maisha yao.

- **Uliza:** Sasa unaweza kutumia YouTube, unataka kuitumia katika nini kwenye maisha yako? (Wape mapendekezo kutokana na wakipendacho)
- **Jadili** na wanafunzi wako ni maneno gani wanaweza kuyatumia kutafuta kutokana na kile wakipendacho (Pendekeza maneno rahisi ya kutafuta na tumia neno 1 hadi 2).
- **Uliza** kila mwanafunzi kuwasha na kuanza kutumia simu kutafuta video anazopendelea na waambie wanafunzi wengine kufanya hivyo.
- **Uliza**: Video gani unataka kutafuta wakati ujao?

**Dondoo:** “Kuna habari nyingi kubwa katika intaneti lakini vile vile nyingine si kubwa na nyingine hazijakamilika kiukweli wake. Ni bora mara kwa mara kuangalia matokeo zaidi ya mara 2 hadi 3 ili kupata jibu sahihi ya unachokitaka.”

# Usalama

**Uliza** “Usalama una maanisha nini kwako?”

**Uliza** wanafunzi wako kufikiria endapo wako katika sehemu ya umati, mfano sokoni. Wambie kujadili watafanyaje kuzingatia usalama katika eneo hili. Waulize maswali yafuatayo na majibu:

| Swali | Jibu sahihi |
|---|---|
| Unafanya nini kama mtu usiyemfahamu anakubugudhi? | Unamuepuka au unamnyamazia. Kuwa makini mara nyingi wanachosema ni tofauti na wanavyoonekana |
| Utafanya nini endapo mtu usiyemfahamu au kumuamini anakuuliza taarifa zako binafsi | Usitoe taarifa zako kwa mtu usiyemfahamu au kumwamini kwasababu anaweza kuzitumia vibaya |
| Unafanyaje kama huna uhakika juu ya jambo unaloliona au ulilozoea kuliona? | Mwambie mtu unayemfahamu na amini juu ya kile kilichotokea |
| Unawachukuliaje watu unaokutana nao? | Kuwa mwema na mtiifu kwa watu |

**Elezea:** “Ni muhimu kukumbuka kwamba intaneti ni sehemu ya wengi na ni muhimu kuchukulia hali hiyo.”


# Usalama




Mpe mwanafunzi wako kitini cha 'dondoo za usalama'.

- **Jadili** na wanafunzi wako maana ya dondoo hizo katika matumizi ya intaneti
- **Lete dondoo hizo katika maisha** kwa kutumia mifano halisi kwa wanafunzi wako. Kwa mfano wanawake wanaweza kuchangia sana juu ya kuzuia usumbufu

## Usalama wa YouTube




- **Uliza** "Kuna chochote kinachokupa wasiwasi unapotumia YouTube?"
- **Uliza** "Kama unapotizama video ya YouTube na ukaona ni mbaya au kosa utafanya nini?"
- **Elezea na onesha kwa vitendo wanafunzi wako** "Unaweza kubonyeza kitufe cha kufuta maneno katika kiboksi cha kutafutia kwa kutumia maneno tofauti"

**Dondoo:** "Una uwezo wa kudhibiti unachokitafuta- Unaweza kutafuta vitu vizuri au unaweza kutafuta vitu vibaya. Ni wajibu wako kutafuta vitu vizuri."

# $ Gharama

**Elezea:** "Sasa unafahamu namna ya kutumia YouTube, na mahala inapoweza kutumika. Ebu tuzungumzie gharama zake kuitumia! Kutumia intaneti katika simu yako, unahitaji kununua data kutoka kwa mtoa huduma ya mtandao, kama unavyofanya katika salio la simu."




## Onesha kipeperushi cha 'gharama'

- **Elezea:** "Vitendo tofauti hutumia kiasi tofauti cha data. Kuangalia maandishi hutumia data kidogo, katika picha hutumia data zaidi. Kucheza na kupakua muziki hutumia kiasi kikubwa zaidi na kucheza hutumia zaidi"
- **Elezea:** "Baadhi ya huduma za intaneti zimeunganishwa katika matukio yanayotumia data zaidi"
- **Uliza:** "Huduma gani inagharama zaidi kutumia?" **Jibu** "YouTube. Kuangalia video za YouTube kunatumia data nyingi"

## Angalia Data

- **Uliza:** "Kwanini ni muhimu kuangalia kiasi cha data ulizotumia? **Jibu:** "Kufahamu ni kiasi gani cha data yako ulichotumia na itakugharimu kiasi gani kwa matukio yote"
- **Elezea:** "Unaweza kuangalia ni kiasi gani cha data unacho, kama vile unavyoangalia dakika au maandishi uliyonayo ; kwa kuandika neno la siri katika simu yako katika mtandao wa simu ya mkononi"
- **Elezea:** "Unaweza kununua za gharama tofauti kulingana na matumizi fulani la Intaneti. Pata ushauri kutoka kwa wakala wako kufahamu ni kiasi gani kinafaa kwako"
- **Elezea:** "Kama unatumia intaneti kupitia Wi- Fi, hautatumia kifurushi chako cha data. Wakala wako atakusaidia kutafuta Wi-Fi iliyoko karibu. Hata hivyo ya ukanda wa karibu inaweza kuwa mbali pia kuifikia"
- **Waoneshe kwa vitendo** wanafunzi wako namna ya kuangalia data zao

**Dondoo:** Yako uliopo na ni mtandao gani pia unatumia katika simu. Mwambie wakala wako akusaidie kuangalia data kama unahitaji.

# Rejea



### Chezea nembo ya mchezo ya YouTube

- **Nyanyua kila** nembo ya YouTube, kila moja kwa wakati wake
- **Uliza** "Hii iko wapi katika simu na ni ya nini?"
- **Elezea** kwa wanafunzi kila nembo ni nini, kama watahitaji msaada
- **Toa zawadi** (Mfano pipi) kwa majibu sahihi na baadaye badika ukutani, kusaidia wanafunzi kujua wao ni akina nani

**Elezea:** Kwamba kuna huduma nyingine zinafanana na YouTube, ambazo zinaruhusu watu kupakia na kuangalia video. Mfano wa hii ni Daily Motion na Vimeo.

**Dondoo:** "Matumizi na huduma katika intaneti hutumia nembo na maneno. Wakati unapotumia intaneti angalia nembo hizi ili kama unazihitaji wakati ujao ujue maana yake."

### Rejea YouTube

**Jadiliana** na wanafunzi wako ni nini wamejifunza kuhusu YouTube

- "Umejifunza nini kuhusu matumizi ya YouTube?"
- "Kuna tofauti gani na TV? Ni kitu gani unaweza kukifanya na YouTube na huwezi kwenye TV?"
- "Bado una lolote kuhusu kutumia YouTube?"
- "Utaitumiaje kwa matumizi binafsi?", "Utaitumiaje kitaaluma?"
- "Unataka kutumia YouTube wapi katika maisha yako, Nini kinakuvutia na kukufurahisha kuitumia?"

**Dondo:** Tumia rejea kama chemsa bongo na toa zawadi (mfano pipi) kwa wanafunzi kwa kucheza.

# Rejea

**Dondoo:** YouTube ina sehemu kubwa kutafuta video, lakini kuna taarifa nyingi zaidi katika inataneti ambazo sio video na ambazo haziwezi kupatikana kupitia YouTube! Intaneti ni kubwa kuliko YouTube, na hata wakati mwingine unaweza kutafuta taarifa kupitia Google".

**Dondoo:** Kama wanafunzi watahitaji kutumia intaneti na YouTube katika simu zao, wape muda fulani kufanya mazoezi ya kile walichokuwa wakijifunza, wape msaada na kuwatia moyo.

## Kwenda kiwango kingine

Kama unatafikia mwisho wa kipengele na bado una muda wa ziada:

- **Uliza:** "Kuna swali lolote kuhusu tulichojifunza katika kipengele hiki?"
- **Uliza** "Kitu gani kingine ungetaka kujua kuhusu intaneti inayotembea?"

---

Vipengele vingine unavyoweza kujadili na wanafunzi wako ni pamoja na:


- **Mchanganuo wa matokeo:** "Unaamuaje kuwa ni video ipi ya kuchagua katika kutafuta kwenye ukurasa wake? Unajuaje kuwa chaguo hili ni bora kuliko jingine?"
- **Kutengeneza Video:** Unaweza kutengeneza video zako pia ukatuma kwa wengine
- **Kutumiana video:** "Kama ungelikuwa na uwezo wa kutuma video yako ya YouTube, ungetuma ipi?"
- **Kupakua apps kutoka** hifadhi yake (utahitaji kuwa na barua pepe kwasababu ni muhimu katika kupakua apps)

# Moduli 4
# Google

# i 4 -
# e

## Malengo ya kujifunza


- Wanafunzi kufahamu namna ya kutumia Google na kutumia yaliyomo katika intaneti.
- Wanafunzi kufahamu ukubwa wa yaliyomo na kuwa na mwamko na hamasa juu ya kutumia uhalisia wa yaliyomo katika intaneti.





**Muda wa kipindi**

Dakika 45-60

## Zana utakazohitaji:




Kalamu, Karatasi na gundi ya karatasi




Simu za Smartphone




Zawadi ndogo




Kipeperushi cha google x1





Vipeperushi vya mkononi




Kipeperushi cha gharama




Dondoo za usalama



Aina za nembo

# Tambulisha Google

## Onesha nembo ya Google kwa wanafunzi na waambie waitafute katika simu

**Uliza** "Kuna anayejua hii?" "Ni ya nini?"

## Toa maelezo mafupi juu ya utafutaji wa Google

- "Google inakusaidia kutafuta taaarifa unazohitaji. Unaiambia Google taarifa unazohitaji kutafuta. Kwa mfano 'Nini ongezeko la watu duniani?' Na itatafuta taarifa zote ambazo zimewekwa na watu kwenye intaneti, kutafuta unachotaka."
- "Unaweza kupata taarifa za mahali, kazi, maelekezo ya mapishi, muvi, nyimbo, habari, taarifa za shule, vyuo, mitihani n. k. "

**Kumbuka:** Husisha mjadala na vitendo wakati wa mafunzo na jinsi ya intaneti inayoweza kuwa msaada katika maisha ya wanafunzi wako. Hii itasaidia kuongeza uhalisia wa mafunzo.

## Lete faida katika maisha!

- **Hadithia** habari yako kwa jinsi utafutaji wa Google ulivyo na faida kwako (mkufunzi), marafiki zako na familia. Mifano iwe na:
- Kutafuta taarifa za sehemu, kazi, watu, watu maarufu, mapishi, muvi, nyimbo, hatari, taarifa za shule, vyuo na mitihani.
- Toa mifano halisi namna ambavyo utafutaji wa Google inaweza kutumika


## Ifanye YouTube kuwa halisia kwa wanafunzi wako

- Jadiliana na wanafunzi wako namna utafutaji wa google unavyoweza kuwasaidia katika maisha yao
- **Uliza:** "Umejifunza nini katika utafutaji kwenye maisha yako." Wape mapendekezo kutokana na wakipendacho
- **Uliza: "**Nini kimekuvutia zaidi na kukuhamasisha katika kujifunza?"

# Kitendo: Matumizi ya awali ya Google


## Fanya mazoezi!

**Elezea** "Sasa unakwenda kujaribu namna ya kutumia utafutaji wa Google katika simu!"




## Onesha namna ya kutumia kippeperushi cha Google


- **Elezea** "Kipeperushi hiki kinaonesha hatua za utafutaji wa Google kupata taarifa"
- Waelekeze wanafunzi kupitia hatua zote katika simu zao zilizounganishwa kwa kutafuta vitu vyepesi.




## Onesha nembo za Google

('Yote', 'maumbo', 'video' na 'ramani')

- **Elezea:** "Unapobonyeza katika nembo tofauti utafutaji wa Google itakuonesha aina tofauti au matokeo au majibu. Kwa mfano ukibonyeza katika nembo ya 'maumbo' utaona maumbo tu, wakati ukitafuta."
- **Uliza** wanafunzi kubonyeza katika nembo tofauti kwenye simu na wakwambie ni vitu gani tofauti wameona walipotafuta.




## Onesha ukurasa wa matokeo kwa nembo 'zote'

('yote', 'maumbo', 'video' na 'ramani')

- **Elezea** ambacho wanafunzi wako wanaangalia: "Google imepewa orodha tofauti ya mitandao ina uhusiano na neno unalolitafuta
- Maandishi ya **Bluu** ni kiunganishi cha kila mtandao, kama ukibonyeza hapo itakupeleka kwenye mtandao
- Maandishi ya **Kijani** ni 'anwani' ya kila mtandao unaishi
- **Maandishi** meusi ni ufafanuzi au chaguo kutoka mtandao huo"

**Uliza** "Una swali lolote kwa kile unachokiona hapa?"

## Kitendo: Matumizi ya awali ya Google

### Nyanyua juu nembo ya Google ya kipaza sauti

- **Elezea** "Kipaza sauti kinaweza kutumika badala ya kuandika maandishi. Wakati ambapo huwezi kutamka au kuandika maneno unayotaka kuyatafuta, unaweza tu Google maneno unayotaka kutafuta "
- **Onesha kwa vitendo wapi pa kuyatafuta:** Nembo ya kipaza sauti itaonekana upande wa kulia wa kiboksi cha kutafutia"
- **Onesha kwa vitendo namna ya kutumia:** "Bonyeza nembo ya kipaza sauti na zungumza kwa sauti safi na taratibu"
- **Wambie** wanafunzi wako kutafuta jina la mtu yeyote maarufu kwa kutumia kipaza sauti.

### Wambie wanafunzi wako kutafuta taarifa kwa kutumia maneno yafuatayo:

1. Andika jina la mtu maarufu katika kiboksi cha kutafutia
2. Andika jina la mahali mashuhuri katika kiboksi cha kutafutia na utafute hapo
3. Wape wanafunzi wako neno 1 la kuandika katika kiboksi cha ambalo linakwendana nao (mfano: basikeli, duka, utaratibu, kazi, kilimo, na wasaidie kutafuta matokeo yake

WIKIPEDIA
Kamusi elezo huru

**Wikipedia** ni mtandao ambao mara nyingi uko karibu na juu kabisa wakati unatafuta kwa Google. Inatoa taarifa katika uwanda mpana. Wikipedia inaandikwa na na watu wanaoitumia na maelfu ya mabadiliko hufanyika kila baada ya saa. Taarifa zake ni muhimu lakini pia unatakiwa kuzipima wewe binafsi kama utafahamu nani alikuwa mwandishi.

## Kitendo: Utafutaji maneno mawili

**Elezea:** "Sasa tunakwenda kujaribu kwa undani utafutaji wa maneno- Hii inaweza kusaidia zaidi kutafuta taarifa unazotaka."

**Wambie** wanafunzi wafanye mazoezi ya kutafuta taarifa kwa kuunganisha maneno 2 hadi 3 katika kiboksi cha Google cha kutafutia. Wanaweza kufanya hivi kwa kutumia kipaza sauti au kuandika katika maandishi. Wape wanafunzi wako maneno tofauti kuyaunganisha, kuzingatia kile walichotafuta awali.

**Dondoo:** Wape muda zaidi wanafunzi wako kupitia matokeo na muungano wa maneno tofauti.

## Kitendo: Utafutaji binafsi

**Jadili na wanafunzi namna ambavyo** Google inaweza kuwasaidia katika maisha yao:

- **Uliza:** "Sasa unaweza kutumia Google, unataka kuitumia katika nini kwenye maisha yako?" (Wape mapendekezo kutokana na wakipendacho)
- **Jadili** na wanafunzi wako ni maneno gani wanaweza kuyatumia kutafuta kutokana na kile wakipendacho (Pendekeza maneno rahisi ya kutafuta na tumia neno 1 hadi 2).
- **Uliza** kila mwanafunzi kuwasha na kuanza kutumia simu kutafuta video anazopendelea na waambie wanafunzi wengine kufanya hivyo.
- **Uliza**: "Video gani unataka kutafuta wakati ujao?"

**Dondoo:** "Kuna habari nyingi kubwa katika intaneti lakini vile vile nyingine si kubwa na nyingine hazijakamilika kiukweli wake. Ni bora mara kwa mara kuangalia matokeo zaidi ya mara 2 hadi 3 ili kupata jibu sahihi ya unachokitaka."

# Usalama

**Uliza** "Usalama unamaanisha nini kwako?"

**Uliza wanafunzi wako kufikiria endapo wako katika sehemu ya umati**, mfano sokoni. Wambie kujadili watafanyaje kuzingatia usalama katika eneo hili. Waulize maswali yafuatayo na majibu:

| Maswali | Majibu sahihi |
|---|---|
| Unafanya nini kama mtu usiyemfahamu anakubugudhi? | Unamuepuka au unamnyamazia. Kuwa Makini mara nyingi wanachokisema ni tofauti na wanavyoonekana. |
| Utafanya nini endapo mtu usiyemfahamu au kumuamini anakuuliza taarifa zako binafsi? | Usitoe taarifa zako kwa mtu usiyemfahamu au kumuamini anaweza kuzitumia vibaya |
| Unafanyaje kama huna uhakika juu ya jambo unaloliona au ulilozoea kuliona? | Mwambie mtu unayemfahamu ukweli na kilichotokea |
| Unawachukuliaje watu unaokutana nao? | Kuwa mwema na mtiifu kwa watu |

**Elezea** "Ni muhimu kukumbuka kwamba intaneti ni sehemu ya wengi na ni muhimu kuchukulia hali hiyo kama mahala pa wengi na salama."


# Usalama




**Mpe mwanafunzi kitini cha 'dondoo za usalama'**

- **Jadili** na wanafunzi wako maana ya dondoo hizo katika matumizi ya intaneti
- **Lete dondoo hizo katika maisha** kwa kutumia mifano halisi kwa wanafunzi wako. Kwa mfano wanawake wanaweza kuchangia sana juu ya kuzuia usumbufu

## Usalama wa Google



- **Uliza** "Kuna chochote kinachokusumbua unapotumia Google?"
- **Uliza** "Kama unapotizama taarifa za Google na ukaona kuwa ni mbaya au ni makosa utafanya nini kifuatacho?"
- **Elezea na kuonesha kwa vitendo kwa wanafunzi wako:** "Unaweza kubonyeza kitufe cha nyuma yake, kufuta maneno katika kiboksi cha kutafutia kwa kutumia maneno tofauti"
- **Elezea** "Unapotumia utafutaji wa Google, unajenga historia ya baadhi ya ulivyotafuta, utakapobonyeza kiboksi cha kutafutia. Kiboski hiki kinaweza kufutwa."


**Dondoo:** "Uko mahala pazuri kwa kile unachokitafuta- Unaweza kutafuta vitu vizuri au unaweza kutafuta vitu vibaya. Ni wajibu wako kutafuta vitu vizuri."

# $ Gharama

**Kama umeshapitia 'Gharama, katika moduli ya Whatsapp na Youtube hapo awali, tumia hii kama ukumbusho**

**Elezea:** "Sasa unafahamu namna ya kutumia Google, na mahala inapoweza kutumika. Ebu tuzungumzie gharama zake kuitumia! Kutumia intaneti katika simu yako, unahitaji kununua data kutoka kwa mtoa huduma ya mtandao, kama unavyofanya katika salio la simu."

---




## Onesha kipeperusi cha 'gharama'

- **Elezea** "Vitendo tofauti hutumia kiasi tofauti cha data. Ukiangalia katika maandishi hutumia data kidogo, katika umbo hutumia data zaidi. Kucheza na kupakua muziki hutumia kiasi kikubwa zaidi na kucheza hutumia zaidi."
- **Elezea** "Baadhi ya huduma za intaneti zimeunganishwa katika matukio yanayotumia data zaidia"
- **Uliza** "Google iko wapi katika kipeperushi? Ina maanisha nini na kiasi gani inatarajia kugharimu?"
- **Uliza** "Ipi ina gharama zaidi? **Jibu** "Video"
- **Uliza** "Ipi ina gharama pungufu? **Jibu** "Maandishi"

# $ Gharama

## Angalia Data

- **Uliza:** “Kwanini ni muhimu kuangalia kiasi cha data ulichotumia?”
- **Jibu:** “Kufahamu kiasi cha data ulichotumia na matukio tofauti yamegharimu kiasi gani”
- **Elezea:** “Unaweza kuangalia kiasi cha data ulichonacho kama vile unavyoangalia kiasi cha dakika au maadishi uliyonayo kwa kuandika neno la siri katika mtandao wa simu yako”
- **Elezea:** “Unaweza kununua data katika viwango tofauti kutokana na matumizi yako ya intaneti. Ulizia ushauri kutoka kwa wakala juu ya kiasi kinachokufaa kwa matumizi yako.”
- **Elezea:** “Kama unatumia intaneti ya WI- FI hutotumia kifurushi chako cha data. Wakala wako anaweza kukusaidia kutafuta ukanda wa WI-FI. Hata hivyo ukanda wa karibu unaweza pia kuwa mabli pia kufikia.”
- **Onesha kwa vitendo** washiriki jinsi ya kuangalia data zao.

**Dondoo:** Uangaliaji wa data utegemea nchi uliopo na simu yako iko katika mtandao gani. Muulize wakala akusaidie namna ya kuangalia data.

# Rejea

## Cheza mchezo wa nembo ya Google

- **Nyanyua** kila nembo ya Google kila moja kwa wakati wake
- **Uliza** “Iko wapi katika simu na ni nini?”
- **Wambie** wanafunzi kutafuta kwa kuangalia umri wa mtu maarufu wanayempenda
- **Toa zawadi ndogo** (mfano pipi) kwa majibu sahihi na bandika nembo ukutani baadaye kuwasaidia wanafunzi kufahamu wao ni nani

# Rejea

**Elezea:** Kwamba kuna huduma nyingine zinafanana na Google ambazo huwawezesha watu wengine kutafuta. Baadhi yake ni Yahoo na Bing.

**Dondoo:** "Matumizi mengi na huduma katika intaneti hutumia nembo na maneno. Unapotumia intaneti angalia hizi nembo, ili ukiziona wakati ujao ujue zina maana gani."

## Rejea kwenye utafutaji wa Google

**Jadili** na wanafunzi juu ya walichojifunza juu ya kutumia utafutaji wa Google

- "Umejifunza nini kuhusu matumizi ya Google?"
- "Bado kuna tatizo lolote kuhusu utafutaji wa Google?"
- "Una matumizi gani binafsi kwa ajili yake? Vipi kuhusu matumizi ya kitaaluma?"
- "Unataka kutumia utafutaji wa Google katika maisha yako? Ni nini kinakuvutia na kukuhamasisha juu ya matumizi yake?"

**Dondoo:** Tumia rejea kama chemsha bongo na toa zawadi (pipi) kwa wanafunzi kucheza.

**Dondoo:** Kama wanafunzi wako watahitaji kutumia intaneti na Google katika simu, wape muda fulani kufanya mazoezi juu ya walichojifunza na wape msaada na hamasa.

# Rejea

## Kwenda katika kiwango kingine

Unapofikia mwisho wa kipengele na una muda wa ziada:

- **Uliza:** “Una maswali mengine ya ziada juu ya lolote tulilojifunza katika kipengele?”
- **Uliza:** “Kitu gani kingine ungependa kufahamu kuhusu intaneti ya simu?”

Baadhi ya viashiria vya ziada ambavyo unaweza kujadili na wanafunzi wako:


- **Tathmini matokeo:** “Unaamuaje kiunganishi cha kutumia kuchagua ukurasa wa kutafutia matokeo?” “Unajuaje kama kama chaguo moja ni bora kuliko jingine?”
- **Kutambua matangazo:** “Unawezaje kutambua matokeo ya Google kuwa yanalipiwa?” “Google inatumiaje historia yako kukuletea matangazo?”
- **Ramani za Google:** “Unatumiaje maelekezo?” “Eneo la Buckingham liko wapi?”
- **Kupakua apps** katika hifadhi yake (Unahitaji kuwa na barua pepe kwasababu kuwa na barua pepe ni muhimu kupakua apps)

# Moduli 5 Wikipedia

# i 5 -
# edia


## Malengo ya kujifunza

- Wanafunzi wanajua jinsi ya kutumia Wikipedia kupata uwelewa wa bure na taarifa.
- Wanafunzi wanaelewa kwamba Wikipedia inaundwa na watu ulimwenguni pote, na wanashikwa na shauku la kuitumia kujifunza mambo mapya.





**Muda wa kipindi:**
Dakika 45-60

## Zana utakazohitaji:




Kalamu, karatasi na gundi ya karatasi




Simu za Smartphone




Zawadi ndogo




Kipeperus hi cha Wikipedia x1




Vipeperushi vya mkononi




Kipeperushi cha gharama




Dondoo za usalama




Aina za nembo

# Tambulisha Wikipedia

## Onesha wanafunzi kipande cha nembo ya Wikipedia

**Uliza:** Kuna yeyote anajua Wikipedia ni nini?" "Inatumikaje?"

**Elezea** kwamba wanafunzi wanawezaje kuingia kwenye Wikipedia kupitia Google kutafuta 'Wikipedia'

## Toa maelezo mafupi juu ya Wikipedia

- "Wikipedia ni rejea ya bure au encyclopedia), inayotupatia taarifa sahihi kuhusu makala ya kuelimisha."
- "Wikipedia ni mtandao. Mara nyingi ni kitu cha awali kuonekana unapotafuta kwenye Google au unaweza kuandika neno 'Wiki' sambamba na maneno unayotaka kutafuta.
- "Wikipedia inaadikwa na watu wa kawaida. Ulimwenguni kote watu hubadilika kila wakati. Unaweza kuhakikisha kuwa taarifa unazozikuta ni za uhakika kwa kuangalia chini ya ukurasa ambapo orodha ya chanzo cha taarifa huwekwa."

**Kumbuka:** Oanisha mijadala na vitendo katika mafunzo namna ambavyo intaneti inavyosaidia maisha ya wanafunzi. Hii itasaidia kuweka uhalisia na kuvutia.

## Kuleta faida katika maisha!

- **Elezea stori yako** ya jinsi Wikipedia inavyokusaidia (Mkufunzi), rafiki yako na familia. Kwa mfano, unaweza kuitumia kwa mtoto wako kufanya kazi zake za nyumbani, Kutafuta majibu ya maswali ya Jiografia au sayansi. Toa mifano husika
- **Uliza** wanafunzi kubadilishana mawazo kwa kile wapendacho. Jibu linaweza kuwa timu ya michezo au mchezo, utamaduni au matukio ya sasa


## Fanya Wikipedia kuwa halisi kwa wanafunzi

- Jadiliana nao jinsi Wikipedia inavyoweza kuwafaidisha katika maisha yao.
- **Uliza** "Ni maswali gani ungependa kujibu kwa kutumia Wikipedia?" Wape mapendekezo kuhusiana na wakipendacho.
    - Michezo (mf. Michezo ya Olimpiki, Kombe la Dunia)
    - Utamaduni wa Pop (mf. muziki)
    - Historia (mf Africa)

# Kitendo: Matumizi ya awali ya Wikipedia


### Fanya mazoezi!

**Elezea** “Sasa unakwenda kujaribu kutumia Wikipedia kwenye simu!”




### Onesha namna ya kutumia Kipeperushi cha Wikipedia

- **Elezea** “Kipeperushi hiki kinaonesha hatua za kutumia Wikipedia kutafuta taarifa.”
- Wapitipshe wanafunzi katika hatua kutumia simu zilizounganishwa na kutafuta mwanamuziki wampendaye.




- **Elezea** wanachokiangalia wanafunzi wako:
- Kila ukurasa unaanza na muktasari wa kile ulicho tafuta.
- Kadri unavyozidi kusoma chini ya ukurasa, utagundua taarifa zaidi historia siasa or Watu wengine walionunganishwa.
- Kila taarifa ina namba mwishoni. Hii inaonana na namba za kumbukumbu kila mwisho wa ukurasa, kuonesha taarifa ilipotoka.

**Uliza** “Una swali lolote kwa hiki tunachoangalia hapa?”

### Onesha wanafunzi jinsi ya kujifunza zaidi juu ya mada.

- **Elezea** “Wikipedia imepangwa kwa mada. Kuna ukurasa wa mwanamuziki umpendaye, lakini pia juu ya muziki katika nchi yako, na kurasa nyingine juu ya muziki wa Marekani.”
- “Kutoka kwenye ukurasa wowote wa Wikipedia, unaweza kwenda moja kwa moja kwenye ukurasa mwingine kwasababu kwasababu kurasa zote za bluu nzima imeunganisha dunia.”
- “Bonyeza katika maneno ya bluu, yatakupeleka kupata taarifa zaidi kuhusu dunia.”
- **Hamasisha** wanafunzi kubonyeza maneno ya bluu katika kila maandishi na kutafuta taarifa zaidi zinazowavutia

## Kitendo: Angalia taarifa

- **Jadili na wanafunzi wako jinsi gani Wikipedia inavyoweza kuwasaidia maisha yao.**

**Elezea:** "Wikipedia huandikwa na watu ulimwenguni kote. Yeyote anaweza kuongeza makala, au kuboresha taarifa. Yeyote anayebadilisha Wikipedia analazimika kuelezea taarifa zimetokea wapi. Hivyo kwamba unaweza kuhakiki mwenyewe ili kuona kama unachosoma ni cha ukweli."

**Waambie** wanafunzi wako kutafuta ukurasa wa Wikipedia wa nchi yao na kisha kusogea chini kabisa ya ukurasa palipo na kumbukumbu.

## Kitendo: Utafutaji binafsi

- **Waambie wanafunzi wako kujizoesha kutafuta taarifa kuhusu mada zifuatazo ndani Wikipedia:**
- Andika jina la nchi yako kweye sehemu ya kutafutia
- Andika jina la mji mkubwa ulio kwenye sehemu ya kutafutia
- Karibisha wanafunzi wako kuandika mada kwenye kisanduku cha kutafutia inayoshabihiana na kile wakipendacho (mf. wanamichezo, burudani, kazi za ujuzi).

**Dondoo:** Watie moyo wanafunzi wako kubonyeza maneno ya blue ya kila kipengere kupata taarifa zaidi yenye mvuto kwao.

- **Wikipedia inapatikana katika lugha mbalimbali:**

**Elezea:** "Wikipedia inapatikana katika takriban lugha 300. Kila moja ikiandikwa na watu wanaoongea lugha husika, hivyo baadhi ya Wikipedia zina makala zaidi kuliko nyingine. Mfano Wikipedia ya Ufaransa ina makala milioni 2, lakini kuna makala zaidi ya milioni 5 kwenye Wikipedia ya Uingereza."

**Onesha** wanafunzi wako kitufe kilichopo juu ya ukurasa kisemacho "Soma kwa lugha nyingine"

# Usalama

**Uliza** "Usalama una maanisha nini kwako?"

**Uliza wanafunzi wako wajihisi kama wako kwenye eneo la watu**, kama vile sokoni. Waulize wangefanyaje ili kuwa salama mahali kama hapa. Watangulizie maswali na majibu yafuatayo:

| Maswali | Majibu sahihi |
| --- | --- |
| Utafanya nini kama kuna mtu usiyemfahamu anakubugudhi? | Muepuke au mnyamazie. Kuwa makini, mara nyingi wanachokisema ni tofauti na wanavyoonekana |
| Utafanya nini endapo kuna mtu usiyemfahamu anakuomba Taarifa zako binafsi? | Usitoe taarifa zako binafsi Kwa usiyemfahamu au kumwamini Sababu zinaweza kutumika kinyume |
| Utafanyaje endapo unahisi huna uhakika Au kuridhika kwa kile unachokiona au kukizoea? | Mwambie unayemfahamu na kumwamini juu ya kilichotokea |
| Unawafanyia nini unajichanganya nao? | Kuwa mtiifu na heshimu watu |

**Elezea** "Ni muhimu kukumbuka kuwa intaneti ni eneo la watu, na ni muhimu kuichukulia kama vile eneo la watu na ubakie salama"

**Usalama kwenye Wikipedia**

**Uliza:** "Kuna chochote kinachokusumbua unapotumia Wikipedia?"


**Uliza:** "Unapotazama kitu fulani kwenye Wikipedia na ukaona kuwa ni mbaya au kosa utafanya nini kifuatacho?"

**Elezea** na onesha kwa wanafunzi wako "unaweza kubonyeza kitufe cha kurudi nyuma na kuendelea kujiunga kwengine ndani ya Wikipedia"

# $ Gharama

**Kama tayari umeshapitia gharama katika moduli iliyopita, tumia hii kama marejeo.**

**Elezea:** "Sasa unajua jinsi ya kutumia Wikipedia, na inaweza kutumika kwa ajili gani, hebu tuzungumzie gharama za matumizi yake! Ili kutumia intaneti kwenye simu yako ya mkononi, ni lazima ununue data kutoka kwa msambazaji wako wa mitandao, kama jinsi unavyofanya kununua muda wa maongezi ya simu."




## Onesha kipeperushi cha 'gharama'

- **Elezea** "Shughuli tofauti hutumia kiwango tofauti cha data. Maandishi hutumia kiwango kidogo, picha zinatumia zaidi, kucheza na kupakua muziki unatumia zaidi kiasi na kucheza video inatumia kiasi kikubwa."
- **Elezea** "Baadhi ya huduma za intaneti zimeunganishwa na kazi zenye kutumia data zaidi"
- **Uliza** "Wikipedia iko wapi katika kipeperushi? Ina maanisha na kugharimu kiasi gani?"

### Kuangalia Data

- **Uliza:** "Kwanini ni vizuri kuhakikisha kiasi gani cha data kilichotumika?"
- **Jibu:** "Ili kuelewa kiasi gani cha data umeshatumia, gharama gani zitatumika kwa shughuli nyingine"
- **Elezea** "Unaweza kuangalia kiasi gani cha data unacho, kama ulivyoangalia dakika ngapi au maneno kwa kuandika namba ya siri kwenye simu simu yako kutoka kwenye mtandao wa simu"
- **Elezea** "Unaweza kununua data kwa gharama tofauti kutegemeana na matumizi yako ya intaneti. Omba ushauri tokwa kwa wakala wa mtandao ili kujua kiasi gani kitakufaa."
- **Elezea** "Kama unapata intaneti kwenye ukanda wa Wi-Fi, hutotumia data yako. Wakala anaweza kukusaidia kupata ukanda wa Wi-Fi. Ingawa ukanda wa karibu unaweza kuwa mbali na mahali ulipo".
- **Onesha** kwa vitendo wanafunzi namna ya kuangalia taarifa zao

**Dondoo:** Uangaliaji wa data unategemea uko nchi gani na mtandao unaotumia. Mwambie wakala akusaidia jinsi ya kuangalia data kama utahitaji

# Rejea



### Chezea nembo ya mchezo wa Wikipedia

- **Nyanyua juu** kila nembo ya Wikipedia, kila moja kwa wakati wake
- **Uliza** "Hii ina kazi gani kwenye Wikipedia?"
- **Elezea** kwa wanafunzi wako maana ya kila nembo kama watahitaji msaada
- **Toa zawadi ndogo** (mf. pipi) kwa majibu sahihi na bandika nembo ukutani baadaye kuwakumbusha nini maana yake

**Dondoo:** Unaweza kukuta kwamba Wikipedia inatokea wakati unatumia huduma nyingine, kama Google au Yahoo, kutafuta intaneti. Mara nyingi Wikipedia ni matokeo ya kwanza ya kutafuta. Unaweza mara nyingi kuona Wikipedia kwanza ili kupata mtizamo mzima wa mada, alafu vinjari tena katika kumbukumbu kutafuta taarifa zaidi iwezekanavyo.

### Rejea kwenye Wikipedia

**Jadili na wanafunzi wako juu ya walichojifunza kuhusu kutumia Wikipedia**

- "Ungezungumziaje Wikipedia kwa rafiki au ndugu yako?"
- "Bado una wasiwasi wowote juu ya matumizi ya Wikipedia?"
- "Ungeitumiaje Wikipedia kwa binafsi au kitaalamu?"
- "Kitu gani hasa kinacho kusisimua unapoingia kwenye Wikipedia?"

**Dondoo:** Endapo wanafunzi wangependelea kutafiti Wikipedia kwenye simu zao wenyewe, wape muda kidogo wa kufanya mazoezi ya kile walichojifunza huku ukiwasaidia na kuwahamasisha.

# Rejea

## Kwenda katika hatua nyingine

**Kama umefikia mwisho wa kipengele Fulani na bado una muda wa ziada:**


- **Uliza:** “Je mna maswali yoyote ya ziada kulingana na kipengele tulichokimaliza?”
- **Uliza:** “Kitu gani zaidi mngependa kukijua kuhusu mtandao wa intaneti?” Baadhi ya viashiria vya kisasa unavyoweza kujadili na wanafunzi ni pamoja na:
- **Pakua App ya Wikipedia. Elezea**, “Unaweza kutafuta moja kwa moja kwenye Wikipedia kwa kwenda kwenye app.”
- **Kujadili:** Kuna jambo la ziada au maswali ambayo yangetakiwa kujibiwa?

# Moduli 6
# Facebook

# i 6 -
# ook




## Malengo ya kujifunza

- Wanafunzi wamejisajili na Facebook
- Wanafunzi wameongeza marafiki, wamefuata kurasa, na wametuma chochote
- Wanafunzi wana shauku la kutumia Facebook na kujiunganisha na marafiki




**Muda wa kipindi:**
Dakika 45-60

## Zana utakazohitaji:

| | | | |
|---|---|---|---|
|  Simu za Smartphone |   Vipeperush i vya Facebook x5 |   Vipererushi mkononi |   Kifurushi cha gharama |
| |   Dondoo za usalama |  Aina za nembo | |

# Tambulisha Facebook

**Onesha wanafunzi nembo ya Facebook na waulize waitafute kwenye simu zao.**

## Toa maelezo mafupi ya Facebook

- "Facebook inakuunganisha wewe na jamii yako, iwe wanaishi karibu yako au mbali nawe. Unaweza kuitumia kwa mawasiliano ya biashara, kupokea habari, kuwasiliana na familia na marafiki au Kwenda sambamba na timu za michezo."
- Ukitumia maneno, picha na video Unaweza kuwasiliana na mtu mmoja mmoja, kundi maalumu la watu au mamilioni kwenye Facebook" specific group of people or millions of people on Facebook."

## Lete faida katika maisha!

- **Simulia hadithi yako,** jinsi unavyotumia Facebook na Inavyokusaidia wewe, marafiki zako na familia. Baadhi ya mifano ijumuishe:
  - Wasiliana na marafiki, familia na mawasiliano ya kibiashara
  - Toa na pokea ushauri
  - Tangaza biashara yako/bidhaa
  - Soma habari za ulimwengu, watu maarufu na michezo

## Toa huduma halisi

Manufaa katika maisha yao:

- **Uliza** "Ungependelea kutumia Facebook kwa ajili gani?" Wape mapendekezo kulingana na mwelekeo wao

# Kitendo: Kuwa na Facebook katika simu

## Fanya mazoezi!

**Elezea:** "Unaweza kupata Facebook kupitia App au web browser."

**Dondoo:** "Ni vyema kupakua na kutumia app ya Facebook kama huna simu ya smartphone na kupata Facebook kwenye web browser kama unatumia simu ya kawaida."




## Onesha kipeperushi "Jinsi ya kupakua Facebook App kwenye simu ya Smartphone"

- Nenda kwenye free.facebook.com/lite au kwenye facebook.com/lite kama ya bure haipatikani
- Bonyeza **Pakua sasa**
- Fungua app ya Facebook Lite
- **Elezea** "Kipeperushi hiki kinaonesha hatua hatua za kufuata kuweza kupakua na kusajili kwenye Facebook"
- Wapitishe wanafunzi wako katika hatua za kufuata kwenye simu zao na elezea kwamba unaweza kuongeza marafiki, kutumamaandishi na picha na kupata habari mpyatoka kwa watu maarufu, timu, timu za michezo, habari na zaidi.

## Onesha jinsi ya kuingia kwenye Facebook katika Web


**Elezea** "Kama una simu ya kawaida unaweza kuingia kwenye Facebook on a web browser."

- Nenda kwenye free.facebook.com au kwenye facebook.com kama ya bure haipatikani
- Wekea alama website ili mwanafunzi aweze kuipata tena

# Kitendo: Fungua akaunti ya Facebook

**Elezea:** "Unahitaji kufungua akaunti ya Facebook ili kwamba marafiki zako waweze kukuona humo.


**Uliza** kama unaweza kusaidia wanafunzi kufungua akaunti na kuwaelekeza kufuata hatua baada ya kwa hatua kwenye kipeperushi




1. Ingiza jina
2. Chagua siku ya kuzaliwa
3. Ingiza namba ya simu ya mkononi
4. Chagua jinsia
5. Chagua namba ya siri iliyo rahisi kukumbuka
6. Pokea na andika namba ya kuthibitisha SMS au WhatsApp
7. Bonyeza "Ok" kuingia

# Kitendo: Ongeza marafiki

**Elezea:** "Lazima uongeze watu kama marafiki kwenye Facebook ili kuona picha na taarifa wanazoziweka na kuweka picha zako na maoni."




## Onesha kipeperushi cha "jinsi ya kuongeza marafiki"

Ongeza marafiki:

- Bonyeza nembo ya marafiki kwa Facebook na elezea mahali zilipo
- Waunganishie wanafunzi angalao marafiki watano ukitumia 'mapendekezo' ya watu unaowafahamu
- Wanafunzi watafute angalao marafiki 2 maalum na kuwaongeza
- Watumie wanafunzi maombi ya rafiki jinsi ya kukubali (au kukataa)
- Elezea kwamba kwa sasa wakati wanapotumia Facebook, wataweza

# Kitendo: Penda vile kurasa za watu maarufu, Michezo na Habari




## Onesha kipoeperushi cha ‘Jinsi yak u-like’ kurasa

- **Elezea** “Unaweza pia kupata habari mpya za watu wako maarufu unaowapendelea, timu za michezo, na habari kwa ku-like kurasa zao. Wakati una “like”kurasa, taarifa wanazozituma zitajitokeza unapojiunga na Facebook.”


## ‘Ku-like’ kurasa:

- Nyanyua juu nembo ya kutafuta na elezea wapi inapatikana
- Uliza wanafunzi ni watu gani maarufu, michezo, habari wanazopendekeza katika kutafuta kisha kwenda kwenye kurasa.
- Waoneshe nembo ya **like** na waoneshe mahali unapobonyeza kwenye kurasa.
- Waoneshe nembo ya **News Feed** na wabonyeze na kuona jinsi mabadiliko

**Dondoo:** Wape muda wanafunzi kutafiti. Acha waongeze marafiki wengi na kurasa kwa kadri watakavyo. Kadri wanavyoongeza zaidi, ndivyo Facebook yao inavyokuwa bora. Unaweza kutuma kurasa zilizo maarufu na eneo husika.

# Kitendo: Fanya kutuma

**Elezea:** “Sasa tujifunze jinsi gani tunaweza kutuma taarifa binafsi au za kibiashara kwenye Facebook.”




### Onesha Kipeperuishi cha ‘Jinsi ya kutuma’

- **Onesha** nembo ya picha/video na wanafunzi waibonyeze
- **Elezea** kwamba unaweza kuchagua nembo ya kamera ili kuongeza picha/video
- **Elezea** kwamba picha au video zinaweza kuongezwa kutoka kwenye simu au nyingine kuondolewa
- **Elezea** kwamba wanaweza kuongeza maandishi kwenye maumbo/video au au kutuma peke yake
- **Elezea** wanaweza kutuma maneno pekee kama hawataki kuchanganya na picha au video.

# Matumizi binafsi

**Jadili** na wanafunzi wako juu ya kile wanachopendelea kutuma kwenye Facebook. Wapatie kile unachotuma kwenye Facebook. Waoneshe baadhi ya yale ulioweka na waambie kwanini umewapatia.

- **Uliza** “Kitu gani ungependa kuwapatia ndugu na marafiki zako?”
- **Uliza** “Kitu gani ungependa kuweka kuendeleza biashara yako?”

# Usalama

**Elezea:** "Kama ilivyo ulimwenguni, kwenye Facebook unaweza kuchagua ni nani unataka kuwasiliana nae na nani hutaki."


**Elezea:** "Picha uliyochagua kama picha ya maelezo yako itakuwa ikionekana kwa watumiaji wote wa Facebook. Hii itasaidia watu kukupata na kukuongeza kama rafiki kwenye Facebook."

**Uliza:** "Unataka kuchagua ili kujua nani anaona picha zako?"

**Onesha kwa vitendo** jinsi ya kuchagua hadhila pale unapoweka picha na jinsi ya kubadilisha mpango wa siri hapo baadae.

**Elezea:** "Unaweza kuweka picha ikaonekana na hadhila(kila atumiae Facebook) au kwa marafiki zako tu."

**Elezea** kwa wanafunzi kwamba wanaweza kuingia na kudhibiti usiri.
**Waoneshe Njia fupi za siri** ambapo wanaweza kuona nani anaweza kuona taarifa zao binafsi, nani wanaweza kuwasiliana kwa maombi ya marafiki, na jinsi ya kuzuia mtu yeyote anayejaribu kuwabughuzi.






# Rejea



### Shikilia kila nembo ya Facebook, kila moja kwa muda wake

- **Uliza:** "Hiki ni kitu gani na kiko wapi ndani ya simu?"
- **Elezea** kwa wanafunzi wako maana ya kila nembo, endapo watahitaji usaidizi
- **Toa zawadi ndogo** (mf. pipi) kwa majibu sahihi na baadae endelea kuonesha nembo ukutani ili kuwakumbusha wanafunzi wako nini maana yake

**Dondoo:** Waache wanafunzi wacheze na Facebook wao wenyewe, kwa kutuma vitu, kubadilishana picha, kutafuta kurasa na kuongeza marafiki. Wahamasishe kuuliza maswali kadri wanavyojivinjari katika Facebook.

### Rejea ya mafunzo muhimu

**Jadili** na wanafunzi wako wamejifunza nini kuhusu matumizi ya Facebook.

- "Umejifunza nini kuhusu matumizi ya Facebook?"
- "Unataka kuitumia vipi Facebook maishani mwako? Kitu gani kinachokufurahisha na kukuvutia unapoitumia?"
- "Utaweka kitu gani baada ya hapo?

# ‘Asante’ & kufunga mafunzo

**Baada ya kumaliza mafunzo, wapongeze wanafunzi wako na watunukie vyeti kama tuzo.**

## Washukuru wanafunzi

- **Uliza** “Mna swali lolote la mwisho?”
- **Shukuru wanafunzi wako:** kwa kutumia muda, mchango na kushiriki kwenye mafunzo

## Wapatie vipeperushi vya mkononi

- **Wapatie wanafunzi wako vipeperushi** kwa ajili ya mafunzo kama hujafanya hivyo
- Hizo ni pamoja na ‘dondoo za usalama’, ’Ufafanuzi’ na ‘WhatsApp, YouTube na Google Jinsi ya kutumia vipeperushi vile vinavyoweza kupatikana kwenye kipengele cha nyenzo cha kitini hiki.







## Fanya sherehe za kufunga

- Mpatie kila mwanafunzi cheti kilichowekwa sahihi(Mfano wa cheti umo ndani ya kipengele cha nyenzo)
- Unaweza pia kuwapatia wakufunzi vyeti vya kumaliza mafunzo “kama wakufunzi”.

**Dondoo:** Unaweza kufanya hivi kwa ajili ya sherehe ya wanafunzi, kwa kuwaomba wafike mbele ya darasa moja

# Aina za vipeperushi na karatasi

# Mwongozo wakati wa mafunzo

## Sehemu hii ni:

### Usalama

Fanya siri taarifa zote za mafunzo haya. Tunapendekeza kutompa mtu namba yako katika makundi

### Jamii inayowasiliana

Kuna watu wenye taarifa tofauti wanakotoka, ufahamu na maoni. Hii ni sehemu yetu ya kuwasiliana, hivyo, heshimu na saidia kila mmoja

### Ukweli & uwazi

Katika maoni yetu na mijadala. Hakuna majibu sahihi au yasiyo sahihi na hatuko hapa kukujaribu

### Usawa

Tutakuwa katika makundi madogo na tutakuwa na simu zilizounganishwa. Tutampa kila mmoja fursa sawa kusikika na kutumia simu

# Dondoo nyepesi kwa usalama wa intaneti



**‘Zuia’ au kataa mtu ambaye humfahamu au anayekubughudhi**



**Hifadhi taarifa zako binafsi**



**Mwambie mtu unayemfahamu na kumwamini, Endapo hauko huru na kile unachokiona au ulichozea**



**Kuwa mtiifu na mwenye kuheshimu watu**

# Ufafanuzi

**Wakufunzi wanaweza kujiongeza katika kipengele hiki kwa kuweka taarifa muafaka kwenye mtandao wa intaneti**

## 2G / 3G / 4G

Intaneti inaweza kwenda kwa kasi tofauti unapoitumia. Intaneti ya 2G ndio kasi ya chini zaidi, 3G ndio intaneti yenye kasi na 4G ni intaneti yenye kasi zaidi kuliko zote.

## App

App inakurahisishia kupata huduma kwenye simu yako.Kwa huduma ya Intaneti mfano,WhatsApp, Facebook, Google, apps inakupatia njia ya haraka na nyepesi kufika kwenye huduma ya intaneti

## Sehemu ya anuani

Hii ni mwonekano wa anuani ya website uliyomo. mf. www.google.in

## Kutangaza au tangazo

Nunua Sasa!

An ad ni sehemu ya taarifa(Tangazo) inayojaribu kukufahamisha jambo fulani. Ni vyema kujizoesha kutobonyeza kwenye tangazo

- Ads(matangazo) yanaweza kuwa video au picha inayojitokeza kwenye kioo cha simu yako.
- Ads(tangazo)yanaweza pia kuwa kiunganishi kinachojitokeza juu yagoogle na upande wa kulia wa kioo cha simu yako.

## Kitafutio

Web browser, au kwa kifupi“browser” ni nyenzo inayotumika kuingia au kuona mitandao. Web browsers zinajumuisha

Google Chrome

Mozilla Firefox

Opera

Microsoft Internet Explorer

## Takwimu

Unapotumia intaneti kwenye simu yako, unatumia kifurushi. Unaweza kununua kifurushi kutoka kwa mtoa huduma za mtandao, kama unavyoongeza salio kwenye simu

## Simu ya kawaida

Hizi ni simu za mkononi zenye uwezo wa kupata intaneti na kuhifadhina uwezo wa kucheza muziki lakini zinakosa nyenzo za kisasa za smartphone

## Google

Google ni huduma ya intaneti inayorahisisha kutafuta taarifa yoyote

# Ufafanuzi

**Wakufunzi wanaweza kujiongeza katika kipengele hiki kwa kuweka taarifa mwafaka kwenyemtandao wa intaneti**

## Intaneti

Intaneti ni mtandao wa mamilioni ya compyuta ulimwenguni uliounganishwa pamoja kupitia laini za simu,setelaite na nyaya. Inakupa wigo mpana wa taarifa na huduma na inaendelea kukua muda wote.Intaneti ni kwa kila mtu.Hakuna kizuizi cha nani anaweza kutumia.Unachohitaji ni kompyuta,simu ya mkononi au tablet na kuunganisha kifurushi.

## Kiungo

Kiunganishi inakuunganisha toka kwenye website moja kwenda nyingine. Kwenda kwenye website nyingine, unaweza kukugusa link na itakuunganisha hadi website nyingine.

## Megabaiti & Gigabaiti

Megabytes (MB) na Gigabytes (GB) ni vipande vya vifurushi unavyotumia wakati unapotumia intaneti. GB ni kubwa x 1000 kuliko MB. Endapo utapakua au kucheza wimbo, ambao uttatumia kiasi kama MB5 (MB 1 kwa dakika)

## Tafuta

Tafuta ni nyenzo inayokusaidia kupata kile unachokitafuta. Unaandika maneno ya kile unacho kitafuta kwenye kiboksi cha tafuta na kisha utaona orodha ya viunganishi kwa Kujibu ya maswali.

## Simu janja

Ni simu ya mkononi yenye uwezo wa kutumia intaneti, kutunza na kucheza muziki na video, na kutumia 'apps'. Simu hizi kwa kawaida huwa zinatumia vi vya kugusa.

## YouTube

YouTube: Ni huduma ya intaneti inayo rahisisha kutafuta, kutazama na kusikiliza video kwenye intaneti. (video tu)

## Mtandao

Taarifa katika intaneti zinahifadhiwa katika mitandao tofauti.Kuna migawanyiko mingi na tofauti kwenye mtandao wa intaneti m.f. Google ni mtandao, YouTube ni mtandao


## WhatsApp

WhatsApp ni huduma ya intaneti inayorahisisha mawasiliano na watu unaowafahamu; familia, marafiki na jamaa.


## WiFi

Ukanda wa WiFi ni eneo ambalo hutumii data zako kuingia katika intaneti ya simu yako; Unaweza kujiunga na intaneti bure. WiFi inapatikana katika baadhi ya maeneo kama mikahawa, na kwenye maduka ya intaneti

# Utangulizi wa Intaneti



# Gharama za Data



Aina za nembo- Apps











Aina za nembo Google






Aina za nembo Google

Aina za nembo YouTube



Aina za nembo YouTube







Aina za nembo Whatsapp

Aina za nembo Whatsapp
















Aina za nembo - Wikipedia











Aina za nembo - Facebook
















# CHETI

Amehitimu

**MAFUNZO YA AWALI YA UJUZI WA INTANETI**

Tarehe

Sahihi



# CHETI

Amehitimu


**MAFUNZO YA AWALI YA UJUZI WA INTANETI**

Tarehe

Sahihi

Namna ya kutumia


# WhatsApp Ujumbe wa mmoja mmoja





Namna ya kutumia

# WhatsApp Ujumbe wa kundi

1 → 2 → 3








WhatsApp

Namna ya kutumia

# WhatsApp Namna ya 'kuzuia'




Namna ya kutumia
# YouTube



Namna ya kutumia


# Google



Namna ya kutumia


# Wikipedia

## Namna ya kubadili Lugha



## Namna ya kutumia

# Wikipedia




Namna ya kutumia


# Facebook

## Jinsi ya kupakua App ya Facebook kwenye Smartphone au kuingia kwenye mtandao


**1**




**2**





**3**



Namna ya kutumia

# Facebook

## Jinsi ya kutengeneza





Namna ya kutumia


# Facebook

## Jinsi ya kuongeza marafiki

1 → 2 → 3







Namna ya kutumia

# Facebook


## Jinsi ya kufuata kurasa


1 → 2 → 3 → 4














Namna ya kutumia


# Facebook

## Jinsi ya utuma

**1** → **2** → **3**



**GSMA HEAD OFFICE**
Floor 2
The Walbrook Building
25 Walbrook
London EC4N 8AF
United Kingdom
Tel: +44 (0)20 7356 0600
Fax: +44 (0)20 7356 0601